**Kampeni** ya Samia yaibua vitendo vya ubakaji kwa watoto

UKURASA 3



RIPOTI MAALUM:

**Uchafu** wa vyoo unavyohatarisha maisha wanafunzi

UKURASA 4




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Julai 30, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581387

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US






DINI NA SIASA:

# CHADEMA yamjibu Msajili wa Vyama

UKURASA 2

"Serikali isimame katika kweli na haki. Hakuna dini inayoruhusu mali za nchi kukabidhiwa kwenye nchi nyingine bila ya kufuata taratibu za kisheria, hivyo lazima wasimame katika kuwatetea wananchi wake." - **MBOWE.**

"Kuna mambo mengi sana hapa tukiyapuuzia, yatakuja kutupa gharama kubwa katika kuyarekebisha. Suala la kuchanganya dini na siasa halina afya kwa taifa." - **JAJI MUTUNGI.**



## CCM yakoleza moto uwekezaji Bandari, yaonya udini, ubaguzi

UKURASA 3

## Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mwanafunzi wa UDOM

UK. 2



Idrisa Mwangobola aliyekuwa akituhumiwa kwa kesi ya mauaji ya mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Happiness Mbonde, akiwa chini ya ulinzi wa Askari Magereza katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam juzi, kabla ya kusomewa hukumu ya kunyongwa hadi kufa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

**MICHEZO** **YANGA YAIUZIA SILAHA AZAM** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji akionyesha Tuzo ya Taasisi Bora ya Udhibiti Barani Afrika kwa mwaka 2023, iliyotolewa na Jarida la African Business Leadership kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na katika hafla ya uwasilishaji jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya TBS, Othmani Chande. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# CHADEMA yamjibu Msajili wa Vyama

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

WAKATI Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, akiviita vyama vya siasa katika mkutano wa dharura kwa lengo la kuwekana sawa kuhusu ushiriki wa viongozi wa dini katika shughuli za kisiasa, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimetoa msimamo wake.

Akizungumza jana katika mkutano wa ufunguzi wa 'Operesheni +255 Katiba Mpya Okoa Bandari Zetu' uliofanyika katika Manispaa ya Bukoba mkoani hapa, Mwenyekiti CHADEMA, Freeman Mbowe, alisema chama hicho hakina dini bali kinaheshimu misingi ya imani ya kila Mtanzania.

Mbowe alisema kila anayehusika katika kudai haki si kwamba ni mwanasiasa bali ni sehemu ya kutetea haki za Watanzania.

Juzi, katika mkutano wake na wahariri wa vyombo vya habari, Jaji Mutungi alitangaza kuitisha mkutano wa dharura wa vyama vya siasa utakaofanyika Jumanne, Dar es Salaam, wenye lengo la kukumbushana sheria na taratibu za nchi ili kufanya siasa bila kuvuruga umoja wa kitaifa.

Jaji Mutungi alisema hivi karibuni kumekuwa na hali ya baadhi ya viongozi wa kidini kushiriki katika shughuli za kisiasa kinyume cha taratibu zilizowekwa kisheria, hivyo kutishia mshikamano wa kitaifa.

Akijibu hoja hiyo katika mkutano wa CHADEMA uliohudhuriwa na mamia ya wananchi na wanachama, Mbowe alisema chama hicho hakiwezi kurudi nyuma katika usimamizi na utetezi wa haki za nchi na wananchi wake.

Mbowe alisema uwapo wa viongozi wa dini katika mkutano huo, unadhihirisha kauli ya kuwa chama hicho hakina udini.

"Serikali isimame katika kweli na haki. Hakuna dini inayoruhusu mali za nchi kukabidhiwa kwenye nchi nyingine bila ya kufuata taratibu za kisheria, hivyo lazima wasimame katika kuwatetea wananchi wake," alisema Mbowe.

Kuhusu uwekezaji, kiongozi huyo aliwataka wanachama na wananchi kuwa na sauti ya pamoja yenye kusimamia maslahi ya umma na kubadili maisha ya Watanzania. Alisema mategemeo ya ujenzi wa nchi ni kwa ajili ya kizazi cha baadaye, hivyo lazima kuwe na uwekezaji wenye tija.

"Katika kulinda rasilimali za taifa, lazima kutengeneza yaliyo mema kwa ajili ya Watanzania na kizazi kijacho, hivyo lazima tusimamie vyema ili kuwa na wawekezaji wenye tija," alisema Mbowe.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, alisema ili kuwapa haki wananchi lazima serikali iweke wazi juu ya maswali yanayoulizwa katika mkataba wa bandari ikiwa ni pamoja na, faida litakazopata taifa kutokana na mkataba huo, ukomo wa mkataba na kutaja mwisho wa shughuli za kampuni hiyo bandarini kama ukomo wa mkataba kuwa si sahihi.

"Ukisema tutanufaika kupitia makusanyo ya TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) si sahihi kwani kama taifa lilishapitia miradi kama hiyo katika sekta ya madini, kwa kile kinachotajwa kuwapo kwa punguzo la tozo kwa wawekezaji kutoka nje, hivyo nchi kushindwa kupata faida ya rasilimali zake," alieleza Lissu.

Alisema chama hicho kitaendelea kutoa elimu kwa umma na kuhakikisha jamii inaelimika juu ya mambo yanayofanywa na serikali ambayo siyo sahihi ili iweze kuchukua hatua.

Lissu alisema elimu hiyo itawasaidia wananchi kuchukua hatua madhubuti ikiwa ni pamoja na kupigania taifa na kukakikisha rasilimali za nchi zipo salama na kufanya uamuzi sahihi wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Kadhalika, alisema kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kuomba mchakato wa haraka wa Katiba Mpya itakayomwondolea vizuizi kiongozi mkuu yeyote pale anapokosea akiwa madarakani.

"Ili taifa kuwa na viongozi wenye nidhamu na rasilimali za wananchi bila kujali wanatokea chama gani, ni lazima tuwe na Katiba pya ambayo itawawajibisha pale wanapofanya kinyume tofauti na sasa, kiongozi anafanya makosa anarudi kuyaandika kwenye vitabu akijua kuwa, hakuna wa kumwajibisha,"alieleza Lissu.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, alisema mtazamo wa chama ni kuanza na upatikanaji wa Katiba Mpya ambayo ndiyo itakayosaidia katika urekebishaji wa sheria mpya za nchi.

Alisema mabadiliko ya katiba yatakuwa chachu ya mabadiliko ya sheria mbalimbali na kueleza kuwa, siyo sahihi kwa sasa serikali kuanza kukimbizana na mabadiliko ya sheria mbalimbali zikiwamo za uchaguzi bali itazamwe kwanza katiba ambayo ni sheria mama.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mwanafunzi UDOM

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA kuu Kanda ya Dar es Salaam, imemhukumu Idris Mwakabola kunyongwa hadi kufa, baada ya kupatikana na hatia ya kumnyonga Happiness Mbonde, aliyekuwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Mwakabola alifikia uamuzi wa kumuua mpenzi wake huyo kwa kuhisi ana uhusiano na mwanamume mwingine. Kabla ya kufanya kitendo hicho, alimwingilia kimwili mpenzi wake huyo bila ridhaa yake kisha kumpa kinywaji chenye kilevi na hatimaye kumnyonga.

Akisoma hukumu hiyo juzi, Jaji Ephery Kisanya, alisema maelezo yanaonyesha kuwa Mwakabola alimuua Happiness baada ya kupata hasira na kwamba kifungu cha 201 cha Kanuni ya Adhabu itatumika, lakini pia maelezo hayo lazima yathibitishe kuwa mauaji yalifanyika wakati mshtakiwa alipokuwa na hasira.

"Lakini lazima mshtakiwa ahojiwe wakati ule ule baada tu ya tukio. Kwa shauri hili, Happiness hakuuawa pale pale baada ya mshtakiwa kuona amepigiwa simu na mpenzi wake wa zamani. hakuna kinachoshawishi kwamba aliuawa kwa hasira, bali inaonyesha Idris (Mwakibola) alidhamiria," alisema Jaji Kisanya.

Jaji Kisanya alisema uchunguzi wa daktari unaonyesha kuwa kifo cha Happiness kilitokana na kukosa hewa kwa kunyongwa na mshtakiwa alimweleza mama yake kuwa mpenzi wake huyo anaumwa huku akijua kabisa si kweli.

Pia alisema hati ya maelezo ya onyo aliyotia saini Mwakabola mbele ya baba yake mzazi wakati akihojiwa na polisi, alikiri kumuua Happiness kwa kumnyonga. Maelezo hayo hakuyapinga mahakamani kwa hiyo mshtakiwa inathibitisha kwamba alitenda kosa hilo kwa kukusudia.

"Baada ya kusikia yote hayo, ili kumtia mtu hatiani lazima mahakama ipitie na kujiridhisha kwa mambo matatu, kama kifo si cha kawaida, kitendo cha mshtakiwa si halali na nia ya mkosaji."

" Swali la kujiuliza je! upande wa Jamhuri umethibitisha hoja namba moja kwa mujibu wa hati ya mashtaka? Hoja hiyo haikubishaniwa na haikupingwa kwani shahidi namba tatu alithibitisha Happiness alifariki dunia kwa kukosa hewa baada ya kunyongwa," alisema

Jaji Kisanya aliendelea kuchambua hukumu hiyo kuwa hakuna aliyemwona mshtakiwa anamuua Happiness, lakini mashahidi wawili kati ya tisa walieleza mshtakiwa alivyokiri kumuua.

Pia alisema shahidi wa tano, ambaye ni Mjumbe wa Serikali ya Mtaa alieleza kushuhudia upekuzi chumbani kwa Mwakabola na kukuta vitu mbalimbali vya marehemu ikiwamo tiketi ya kusafiria ya basi la Kimbinyiko.

Jaji Kisanya alisema shahidi namba saba, Sajenti Samuel wa kitengo cha upelelezi Kigamboni, aliwasilisha taarifa ya uchunguzi wa daktari kuhusu kifo hicho na kuthibitisha pia kuwa tiketi ya basi iliyokutwa ilikuwa ya marehemu Happiness.

Alisema ushahidi wa shahidi namba nane, Brass Kaijango, kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, aliyechukua sampuli za vinasaba kutoka kwenye kiatu aina ya sandoz iliyokutwa kwa mshtakiwa na kulinganisha na mama mzazi wa marehemu, pia umethibitisha bila shaka uhusiano wao.

Jaji Kisanya alisema mshtakiwa katika maelezo yake alisema vielelezo vyote vililetwa kwake na polisi, lakini saini ya mshtakiwa huyo ilithibitisha kuwa vitu hivyo vilikutwa kwake.

"Kutokana na maelezo yote na vielelezo, tiketi na sandos, pia mshtakiwa alimwingilia Happiness bila ridhaa, sioni sababu ya kutokuamini ushahidi ulitolewa na vielelezo kupatikana kwa mshtakiwa; tena maelezo ya kukiri ya Idrisa yametolewa mbele ya mtu thabiti, (baba yake mzazi)," alieleza Jaji Kisanya.

"Idrisa umetiwa hatiani kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu ya mwaka 2019 toleo la 2020 na unahukumiwa adhabu ya kifo kwa kunyongwa na pia kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 223, mshtakiwa una haki ya kukata rufani ndani ya siku 30," alisema.

Kabla ya kutoa hukumu hiyo, Jaji Kisanya alitoa nafasi kwa Wakili wa Serikali, Salome Matunga akisaidiana na Upendo Mono na Aziza Mhina, ambao waliiomba mahakama kwa busara zake impe adhabu inayomstahili, kwa sababu mauaji aliyoyafanya ni ya kikatili na hayaelezeki.

Wakili wa utetezi, Hilda Mushi, aliyemwakilisha Wakili Godfrey Albert, aliiomba mahakama impunguzie adhabu mshtakiwa kwa kuwa bado ni kijana mdogo anayetegemewa na familia yake na ni nguvu kazi ya taifa. Baada ya hukumu hiyo kutolewa, mshtakiwa alianza kutiririkwa na machozi, huku mama yake na ndugu wengine wakiangua kilio mahakamani.

Tukio hilo la mauaji lilitokea Machi 18, 2019 wakati Happiness akijiandaa kurejea chuoni kwa masomo. Siku hiyo alikwenda kukata tiketi ya basi la Kimbinyiko kwa ajili ya kusafiri siku inayofuata lakini alikutana na Idrisa anayedaiwa alikuwa mpenzi wake na kwenda naye nyumbani kwao, Kigamboni.

Happiness hakurudi nyumbani hadi mwili wake ilipookotwa maeneo ya Buza Relini usiku huo wa Machi 18, 2019 baada ya kutupwa na mshtakiwa. Ulitambuliwa na baba yake mzazi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Temeke baada ya kuarifiwa na polisi kuwa kuna miili ya watu wawili imeokotwa maeneo tofauti wilayani Temeke.

# CCM yakoleza moto uwekezaji bandari

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amekoleza moto wa uendeshaji wa Bandari kupitia mwekezaji, kampuni ya DP World na kusisitiza kuwa serikali haitarudi nyuma.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Dar es Salaam, Chongolo alisema wanaopinga uwekezaji huo wanafahamu wanachofanya isipokuwa wanasubiri CCM irudi nyuma wapate hoja ya kusimamia kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Mkutano huo ni miongoni mwa mikutano iliyofanyika katika kanda saba kueleza utekelezaji wa Ilani ya CCM na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

Juzi, viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakiongozwa na Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe na Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu, walifanya mkutano wao wa hadhara mkoani Kagera kupitia kampeni ya Operesheni Komboa Bandari, ikilenga kupinga uwekezaji huo.

Chongolo alisema: "Lazima tutende tunayoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi ya 2020 -2025 kwa sababu dhamira yake ni kuhakikisha tunapata fedha za kutosha ili kukimbiza utekelezaji wa ilani na kutatua changamoto za wananchi.

"Suala la bandari wapinzani wanafahamu kuwa wameshikwa pabaya kwa sababu wanafahamu ukitekelezwa, serikali itapata fedha za kutoka kupitia bandari kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo."

Alisema wapinzani wamezungumza hoja za uongo na kwa sasa wameamua kuingia kwenye matusi baada ya kuona chama tawala kinajibu hoja zao.

"Upinzani wanaeleza hoja zao na CCM nayo inabaki kwenye hoja zake za msingi na hakitajihusisha na kwenye hili la Bandari serikali itaendelea na mchakato wake kwa kusikiliza maoni ya watu wenye nia njema ya kujenga," alisisitiza Chongolo.

Alisema CCM ndicho chama kinachoongoza nchi kwa kushika usukani na lazima waonyeshe ujasiri wa kuendesha nchi kwa kuwa wana dhamana hiyo na kwamba suala la upinzani kuanza kuzungumzia hoja za ubaguzi ni dhambi kubwa.

Alisema wamekosa hoja za msingi ndiyo sababu wanajenga hoja za kibaguzi (bila kuutaja) hali itakayoleta chuki ndani ya jamii na taifa kwa ujumla.

"Ukiona adui yako anakushangilia wakati unafanya jambo, achana nalo kwa sababu halina maana lakini ukiona anakupiga vita endelea mbele kwa sababu lina manufaa makubwa," alisema Chongolo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, aliwatolea uvivu wapinzani wanaoibeza serikali kuwa imegawa nchi kwa kuuza bandari kuwa hawajui wanachokisema.

Alikataa pia kuwa wanaodai mkataba wa bandari ni mbaya kuliko yote iliyowahi kutiwa Saini nchini ni waongo na hawana ushahidi.

Prof. Mkumbo ambaye pia ni Mbunge wa Ubungo, alibeza mkutano wa CHADEMA uliofanyika mkoani Kagera juzi kwa madai kuwa umedhihirisha udhaifu wao wa kukosa hoja za msingi na wananchi wa kuwasilikiza.

Alisema mkataba huo unahusu Bandari ya Dar es Salaam na mwekezaji anapewa asilimia kidogo na sehemu ya eneo na siyo bandari yote kama ambavyo wapinzani wanadanganya wananchi.

"Kimsingi hoja za kitaalam na za kisera zimeshajibiwa na hoja zilizobaki ni za kisiasa. Hoja za kisheria na za kitalaam zote zimejibiwa kiufasaha na za kisiasa zitajibiwa kisiasa," alisema Mkumbo.

Alifafanua kuwa serikali ina dhamira njema ya kusaidia wawekezaji nchini na imejipanga na kuweka mazingira wezeshi.

Mwanasiasa mkongwe, Stephen Wassira, alisema wanaopinga hoja ya bandari ni wale wanaonyemelea urais na wale ambao walikuwa wanadhani Rais Samia atashindwa kuongoza nchi. "Sasa wanajiuliza kufikia uchaguzi mkuu wa 2025 watamsemea wapi? Maeneo yote amefanya vizuri na ndiyo sababu wakaona wamzulie jambo kuwa ameuza bandari, mara ameuzwa nchi.

"CCM haiwezi kuuza nchi na wala haitafikia mikononi mwa CCM kwa sababu sisi ndio tuliodai uhuru wa nchi hii na waasisi waliiacha mikono salama nchi hii," alisema Wassira.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo akihutubia wananchi na wanachama wa chama hicho, katika viwanja vya Tanganyika Packers Kawe, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kampeni ya Samia yaibua vitendo vya ubakaji, ulawiti kwa watoto

**Na Ibrahim Joseph,** SONGEA

KAMPENI ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia imewaibua wazazi wa watoto wanane waliofanyiwa vitendo vya ulawiti na ubakaji katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Wazazi hao walitoa kilio hicho juzi walipokutana na timu ya huduma ya msaada wa kisheria inayoendelea na kazi maeneo tofauti tofauti mkoani hapa.

Mmoja wa wazazi hao (jina linahifadhiwa) alisema mtoto wake ni miongoni mwa watoto wanane waliofanyiwa kitendo hicho tangu Machi, mwaka jana.

Mzazi huyo alisema watoto wote waliofanyiwa vitendo hivyo ni wakazi wa Mtaa wa Seedfarm katika Manispaa ya Songea na mtuhumiwa anayedaiwa kufanya vitendo hivyo ni mkazi wa mtaa huo jirani na wanapoishi.

Mzazi huyo alimtaja mtuhumiwa anayedaiwa kuwafanyia watoto hao vitendo hivyo kuwa ni Sabri Milanzi ambaye alikuwa kiwafanyia vitendo hivyo nyumbani kwa wazazi wake.

Alibanisha kuwa taarifa za watoto hao kuhusu kufanyiwa vitendo hivyo wazazi, walipewa na walimu wa shule wanayosoma baada ya kuona hali zao wakiwa kuwa si kama zilivyozoeleka.

Baada ya walimu kuzungumza na mmoja wa watoto, alisema ukweli kuhusu kufanyiwa kitendo hicho na mtuhumiwa anayedaiwa kuwafanyia hivyo mara kwa mara. Aliongeza kuwa baada ya mazungumzo hayo, mtoto aliwataja na wenzake wengine saba ambao wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo na mtuhumiwa na amekuwa akiwatishia kuwa wakisema kwa wazazi wao atawaua, hivyo walikuwa wanaogopa.

Aliongeza kuwa baada ya hapo, walimu walichukua jukumu la kuwaita wazazi wa watoto hao na kuwaeleza taarifa za wanafunzi hao waliobanika kufanyiwa vitendo hivyo na kwamba baada ya kupewa taarifa hizo wazazi hao waliungana na kutoa taarifa Kituo Kikuu cha Polisi Songea na wakaendelea na taratibu za kuwapeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Songea ambako walidai kupewa majibu ya vipimo kuwa watoto wako salama.

Kwa mujibu wa mzazi huyo, wote hawakuridhika na majibu hayo ya madaktari, hivyo ikabidi wachukue hatua ya kupewa gari na Jeshi la Polisi kwenda Hospitali ya Misheni ya Peramiho na vipimo vilionyesha kuwa watoto hao walifanyiwa vitendo hivyo.

Baada ya majibu hayo, alisema walirudi polisi na kutoa taarifa hizo kisha kujibiwa kuwa jeshi litafanya utaratibu wa kumtafuta mtuhumiwa ili sheria ichukue mkondo wake lakini mpaka sasa hawajapata taarifa za kukamatwa kwake.

Pia alisema, cha kusikitisha ni kuwa jeshi hilo limekaa kimya na hakuna kinachoendelea na ndipo waliposikia taarifa za uwapo wa kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia mkoani Ruvuma, hivyo wakafika kuomba msaada wa kisheria kuhusu tukio hilo.

**WAZAZI WA MTUHUMIWA**

Nipashe ilizungumza na mzazi wa mtuhumiwa anayedaiwa kufanya vitendo hivyo, Abdul Milanzi, ambaye alisema taarifa kuhusu madai hayo walipewa na polisi baada ya kukamatwa na kuulizwa aliko mtoto wao.

Milanzi alisema baada ya kukamatwa walikaa mahabusu wiki moja yeye na mke wake lakini wakadhaminiwa na kupewa masharti ya kushirikiana na jeshi hilo kumtafuta mtuhumiwa lakini mpaka sasa hawajui alikokimbilia. Alisema wamefanya juhudi za kuwatafuta kwa ndugu zao lakini hawajampata.

**KAULI YA RPC**

Timu ya waandishi wa habari ilimtafuta Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Kamishna Msaidizi (ACP) Alfred Hussein, ambaye alisema Machi 23, 2022 ilipokea taarifa katika kituo cha Songea kuwa watoto wanane , wa kiume saba na wa kike mmoja wenye umri tofauti kuanzia miaka sita hadi 12, walifanyiwa vitendo vya ulawiti na ubakaji katika Mtaa wa Making'inda, Manispaa ya Songea.

ACP Hussein alisema baada ya vipimo na uchunguzi wa madaktari, ilibainika kuwa watoto wanne walionyesha dalili za kulawitiwa na mmoja wa kike kubakwa na watoto watatu hawakuonyesha dalili za kufanyiwa vitendo hivyo.

Alisema watoto wawili miongoni mwa hao wanne waliolawitiwa, walimtaja Jackson Peter, mkazi wa mtaa wa Making'nda kuwa ndiye amewafanyia vitendo hivyo na watatu waliobaki akiwamo mtoto wa kike, walimtaja Sabri Milanzi ambaye alitoroka baada ya kusikia anatajwa kuhusiana na tuhuma hizo.

Kamanda alisema mtuhumiwa Jakson Peter (17) alikamatwa na polisi na kufikishwa mahakama ya watoto kwa tuhuma za kulawiti na kuhukumiwa viboko vitatu kwa kila kosa, hivyo alitumikia adhabu ya viboko sita kwa makosa hayo.

Pia alisema juhudi za Jeshi la Polisi kumtafuta mtuhumiwa Sabri Milanzi zinaendelea na atakapokamatwa atafikishwa mahakamai kujibu tuhuma zinazomkabili.

Kampeni ya huduma msaada wa kisheria ya Mama Samia, ilizunduliwa mkoani Ruvuma Julai 22, mwaka huu, na Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango na inaendelea maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Lengo la kampeni hiyo ni kutoa elimu na kutatua matatizo ya migogoro na kero za wananchi kwa nchi nzima.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**JESCA FRANCIS MONGI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 491 DDQ.** Chassis namba **NCP600123358.** Engine namba **2NZEAA3358.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/207962/2023.**

# Uchafu vyoo unavyoweka hatarini maisha wanafunzi

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

HALI si shwari kwa wanafunzi na walimu. Ndivyo hali halisi ilivyo kutokana na kilio cha wanafunzi wa shule kongwe za msingi katika Manispaa ya Kigoma Ujiji kutokana na kuwa katika hali ya hatari inayowakabili.

Kwa mujibu wa wanafunzi wanaosoma shule za msingi za Lake Tanganyika na Kigoma, katikati ya mji wa Kigoma, wako katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya kuambukiza kutokana na uchafu uliokithiri katika vyoo vya shule hizo.

Licha ya kuwapo kwa uchafu pia vyoo hivyo, kilio kingine cha wanafunzi hao ni ukosefu wa maji, hivyo kuwalazimu kutumia makaratasi kujisafisha huku wengine wakiamua kujisaidia nje ya vyoo na wengine mtaroni ambako hujisafisha kwa kutumia maji yanayopita katika mtaro huo ulioko pembeni mwa shule hizo.

Hamisi Issa, mwanafunzi wa darasa la nne kutoka Shule ya Msingi Lake Tangayika, alisema mabomba kwa ajili ya kutoa maji yapo japo hayafanyi kazi na ndoo zilizopo chooni ni chache hazikidhi mahitaji ya wanafunzi waliopo ndiyo maana wanaamua kujisaidia na kujisafisha kwa kutumia makaratasi.

Naye Latifah Shaaban, mwanafunzi wa darasa la nne kutoka Shule ya Msingi Kigoma alisema wanasafisha vyoo kila siku lakini wakienda chooni wanakutana na uchafu ukiwa umezagaa juu ya choo. Alisema hali hiyo inawafanya kuona kinyaa na kuamua kujisaidia haja kubwa na ndogo nje.

Mwanafunzi mwingine, Haidari Jumanne, wa darasa la saba kutoka Lake Tanganyika, alisema kutokana na hali ya uchafu, wanapatwa na magonjwa ya homa za matumbo, maambukizi kwa njia ya mkojo (UTI) na kuwashwa sehemu za siri (fangasi) hali inyoongeza gharama za matibabu.

Kutokana na hali hiyo, wanafunzi hao wamewaomba wazazi kujitolea mchango ili kuhakikisha kunakuwa na maji ya kutosha na vifaa vya usafi ili kuweka vyoo katika hali ya usafi.

Ongala George, mwanafunzi wa darasa la saba Shule ya Msingi Kigoma, alisema maji ya kisima yalipoko shuleni kwao si masafi na miundombinu ya chooni si mizuri ndio maana baadhi yao wanaamua kujisaidia nyuma ya vyoo ili kuepuka uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa.

### KAULI WALIMU WAKUU

Akijibu malalamiko ya wanafunzi, Mwalimu Mkuu wa Lake Tangayika, Lunuguye Kalabona, alisema vyoo vinachafuliwa na watu wa mitaani, kama mateja na wavuta bangi kwa kuwa wanakosa pesa ya kulipia kwenye vyoo vya stesheni ya reli.

Kwa mujibu wa mwalimu mkuu huyo, shule yake ina wanafunzi 339 na vyoo vinane, vinne kwa watoto wa kike na vinne kwa watoto wa kiume ambavyo vinatosheleza mahitaji, hivyo isingekuwa rahisi kwa vyoo kuchafuka kwa kiasi kikubwa kwa kuwa vinasafishwa kila siku asubuhi kabla ya kuanza masomo.



Ili kutatua kero hiyo, Kalabona alisema wameamua kushirikiana na Umoja wa Wazazi na Walimu (UWAWA) na kukubaliana kuanza kuchanga Sh. 10,000 kila mzazi ili kupata Sh. milioni 2.5 zitakazowawezesha kujenga uzio na kununua milango ya magrili ambayo itakuwa suluhisho la kudumu.

Naye Bujaga Simon, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kigoma alisema sambamba na mwingiliano wa jamii, shule ina upungufu wa matundu 22 ya vyoo kwa kuwa ina wanafunzi 785, hivyo matundu tisa yaliyopo hayakidhi mahitaji ya uwiano wa tundu moja kwa wanafunzi 25 wavulana na tundu moja kwa wanafunzi 20 kwa kike.

Alisema pamoja na vyoo kusafishwa asubuhi na saa 6:00 mchana, bado vyoo vinakuwa vichafu kwa kuwa havina mifumo ya maji na vifaa kwa ajili ya kusafisha pamoja na kutunzia maji. Hali hiyo alisema inawafanya wanafunzi kuchota maji kisimani na kwenda nayo chooni na kuwa mwanafunzi aliyekanwa na haja, inakuwa ngumu kukumbuka kubeba maji.

Ili kupata suluhusho la kudumu, Mwalimu Simon aliiomba serikali na mamlaka za elimu nchini kuwawezesha kujenga uzio ili kudhibiti mwingiliano wa jamii unaosababisha uchafuzi wa mazingira na wizi wa vifaa vya usafi shuleni. Pia aliomba msaada wa mapipa ya kutunzia maji karibu na vyoo pamoja na kuwanunulia vifaa vya usafi.

### VIONGOZI WAIBUKA

Ofisa Elimu ya Awali na Msingi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, Richard Mtauka, alisema kero hizo zinafahamika na tayari mikakati ya utatuzi imeanza kwa kufanya vikao na wazazi ili kuwahamasisha kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya shule zao. Alisema hali itakayosaidia kupunguza kero hizo wakati serikali ikijipanga kuweka uzio kwa shule zote kongwe na za kisasa.

"Halmashauri imetenga Sh. milioni 100 kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa ajili ya kujenga uzio katika shule zote 46 ili kuwaweka watoto salama na mbali na mwingiliano wa jamii. Vilevile manispaa ina bajeti ya Sh. milioni 92 ambayo itatumika kuweka miundombinu ya maji vyooni na mpaka sasa barua ya kuomba huduma ya maji ishapelekwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma (KUWASA) ili maji yatoke shuleni bila kukatika kutokana na mgawo," alibainisha Mtauka.

Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Salum Kali, aliwaagiza wakuu wa idara, wakurugenzi na maofisa elimu wa Halamsahauri ya Wilaya ya Kigoma na Manispaa ya Kigoma Ujiji kuanza maandalizi ya kujenga uzio kupitia wazazi ili kuwalinda watoto dhidi ya hatari kutoka kwa watu ambao si waaminifu kwa kuwa kutakuwa na uangalizi mkubwa kujua nani anaingia na nani anatoka.



**Picha ya juu ya chini:** Ni Hali halisi ya vyoo katika shule za msingi Lake Tanganyika na Kigoma. **PICHA: ADELA MADYANE**

HABARI KITAIFA

# Russia yaahidi kuboresha uchumi Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ya Russia imeahidi kushirikiana na Afrika kuboresha uchumi ikiwamo Tanzania.

Majaliwa aliyasema hayo juzi baada ya kumalizika kwa Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka mataifa ya Afrika na Russia, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, mkutano huo ulifanyika kwenye kituo cha mikutano na maonyesho cha Expo Forum, jijini St. Petersburg, Russia.

"Mwelekeo wa mkutano wa leo (juzi) ulikuwa kuona namna gani tunaweza kuboresha uchumi wa nchi za Afrika kwa pamoja na Russia. Wao wametoa mwelekeo wa namna ambavyo wataweza kushirikiana na nchi za Afrika kuboresha uchumi wa kila nchi na sisi tumeeleza mkakati wa kiuchumi kwenye nchi yetu ambao Rais Vladmir Putin ameuridhia," alisema.

Waziri Mkuu alisema Tanzania itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji kwa lengo la kuboresha uchumi na biashara kwa kutumia rasilimali zake ikiwamo madini, maliasili na kilimo hasa upatikanaji wa mbolea.

"Tumesisitiza pia, matumizi ya nishati mbadala kama njia muhimu ya kuwawezesha wananchi wa vijijini ili nao wamudu kutumia nishati mbadala kukuza uchumi wao," alisema.

Alilitaja eneo lingine kuwa ni kukuza biashara ya mazao baina ya Afrika na Russia na kwamba yenyewe inaweza kuwa soko la moja kwa moja au kwa kuwatumia marafiki zake. "Ili kufikia hayo, jitihada za kila nchi kwenye kilimo zimesisitizwa. Tanzania tumeeleza mkakati wa kukuza kilimo ikiwamo umwagiliaji. Pia tunahitaji mbolea, dawa na vitendea kazi ili tufanikiwe kwa kasi zaidi," alisema.

Waziri Mkuu aliwaeleza viongozi hao wa Afrika juu ya Mkakati wa Rais Samia wa kutoa elimu bure na vifaa vya kufundishia kwa lengo la kuwapunguzia mzigo wazazi.

Akifungua mkutano huo, Rais Putin alisema nchi za Afrika zimekuwa na uhusiano mzuri na wa muda mrefu na Russia na kwamba nchi hiyo imekuwa ikiendelea kutoa misaada bila vikwazo kwenye maeneo mbalimbali.

Rais Putin alisema nchi 40 kutoka Afrika zimenufaika na misaada ya kijeshi ikiwamo mafunzo.

"Ukaribu wa uhusiano kati ya Afrika na Russia unazidi kuongezeka. Tunatarajia kufungua balozi zetu kwenye nchi nyingine kama vile Burkina Faso na Equatorial Guinea. Pia tunatarajia kufufua vituo vya utamaduni vya Kirusi. Hivi sasa, vituo kama hivyo vinafanya kazi kwenye nchi nane tu," alisema.

Kiongozi huyo alisema nchi hiyo itaendelea kutoa misaada kwenye sekta ya kilimo ili kuimarisha upatikanaji wa chakula.

"Jana ndiyo maana nilitoa ahadi ya kuzipatia nafaka nchi sita, tani kati ya 25,000 hadi 50,000 na kwamba zitasafirishwa bure. Nchi hizo ni Mali, Burkina Faso, Zimbabwe, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Eritrea na Somalia," alisema.

Alisema Russia imepanga kutoa Dola za Marekani milioni 90 kwa nchi za Afrika kulingana na maombi ambayo yamepokewa kutoka Umoja wa Afrika (AU).

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni alisema mwishoni mwa mkutano huo watoke na tamko la kisera ya kwamba mataifa ya nje yanapaswa kununua kutoka Afrika bidhaa zilizosindikwa badala ya mazao ghafi.

"Napendekeza tutoke na tamko la kisera kwa nchi zote kwamba wakija kwetu wanunue chokoleti badala ya kakao, kahawa iliyosindikwa badala ya ghafi na bidhaa za chuma zilizosanifiwa badala ya chuma ghafi," alisisitiza.



Baadhi ya madiwani wanawake kutoka wilaya za Kaskazini A na B, Mkoa wa Kaskazini Zanzibar, wakijifunza kutengeneza mkaa mbadala walipofanya ziara ya mafunzo katika Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Tani milioni 3.7 saruji Tanzania zauzwa nje

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema takwimu za uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2022 zinaonyesha ziada ya tani milioni 3.75 imeuzwa katika soko la nje ya nchi.

Akizungumza juzi kuhusu mwenendo wa bei za bidhaa muhimu, Dk. Kijaji alisema saruji hiyo inauzwa katika nchi za Jamhuri ya Kidemorasia ya Congo (DRC), Rwanda, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji.

"Hadi kufikia Juni, mwaka huu, Tanzania ina viwanda vya saruji vipatavyo 14. Kati ya hivyo, viwanda saba ni vikubwa na vilivyobakia vinazalisha saruji kutokana na malighafi (clinker) iliyozalishwa na viwanda hivyo saba.

"Takwimu za uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2022, zinaonyesha kuwa viwanda vya saruji nchini vinazalisha tani 10,850,000 za saruji kwa mwaka na mahitaji ya ndani ya nchi ni tani 7,100,000 kwa mwaka. Hivyo, kuna ziada ya tani 3,750,000 ambazo huuzwa katika soko la nje hususani Congo, Rwanda, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji,"alisema.

Hata hivyo, alisema kuanzia Julai, 2022 hadi Juni, mwaka huu, uchambuzi unaonyesha saruji aina ya 32.5R iliuzwa kwa Sh. 17,009 kwa mfuko wa kilo 50.

"Wastani wa bei ya chini ya saruji ya aina hiyo nchini kwa kipindi hicho ilikuwa Sh. 14,203 huku Julai, 2022 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Sh. 12,500 kwa mfuko wa kilo 50," alisema.

Pia alisema saruji ya aina ya 42.5R, uchambuzi unaonyesha kuwa kwa mwaka 2022/23 wastani wa bei ulikuwa Sh. 18,217 kwa mfuko wa kilo 50.

"Wastani wa bei ya chini katika kipindi hicho ulikuwa ni Sh. 14,917 kwa mfuko wa kilo 50 huku Julai 2022 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Sh. 13,500 kwa mfuko wa kilo 50," alisema.

Alibainisha kuwa wastani wa bei ya juu ilikuwa Sh. 23,800 kwa mfuko wa kilo 50 na miezi ya Aprili, Mei na Juni, 2023 ikiwa na bei ya juu kuliko miezi yote kwa Sh. 24,500 kwa mfuko wa kilo 50.

# ACT Wazalendo yatamba ina watu makini wa kuongoza nchi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu, amesema chama hicho kiko tayari kushika uongozi wa nchi kwa kuwa kina watu makini wa kutekeleza majukumu yote ya kiserikali bila ya kuyumba.

Shaibu alitoa kauli hiyo jana Bagamoyo, mkoani Pwani, wakati akitoa mada kwenye mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo mawaziri vivuli wa chama hicho ili kufanya kazi kwa ubora zaidi, pamoja na tathmini ya mwaka mmoja tokea baraza hilo lilipoasisiwa kwa ajili ya kuisimamia serikali.

Alisema wakati Halmashauri Kuu ya Chama hicho ilipokutana Januari 28, 2022 na kuazimia kuundwa kwa kamati ya kuisimamia serikali nje ya Bunge, maoni ya watu wengi yalikuwa kama kamati hiyo itaweza kuziba ombwe la wasemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ndani ya Bunge, suala alilosema baaada ya mwaka mmoja, maswali hayo yameisha na chombo hicho kugeuka kuwa tegemeo la watu mbalimbali katika kuisimamia serikali.

"Mimi ndiye mtendaji mkuu wa chama chetu. Kwa sasa na nina nafasi nzuri ya kuelezea mafanikio ya Baraza Kivuli la ACT Wazalendo tokea kuanzishwa kwake. Ninaomba niwaambie kwa namna mnavyoshughulikia na kutoa majawabu ya masuala mbalimbali ni wazi sasa tumeiva kushika dola na kuiongoza kwa ufanisi mkubwa sana,"alisema Shaibu. Aliwataka mawaziri vivuli wanaohudhuria mafunzo hayo ya kujengeana uwezo, watumie nafasi hiyo kufanya kazi kwa umakini zaidi kwa lengo la kuiaminisha jamii.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Juma Duni Haji, alisema Tanzania inaumizwa kutokana na viongozi wanaopewa dhamana ya uongozi kutokuwa waadilifu na kutoheshimu taratibu na malengo yaliyowaweka madarakani.

Alisema malalamiko mbalimbali ya uadilifu unaolalamikiwa serikalini kwa kiasi kikubwa, umechangiwa na viongozi wa ngazi za juu kutokuwa waadilifu.

"Kiongozi unatakiwa uwe mfano kwa wengine, ukisimama katika uadilifu na kuheshimu sababu zilizokuweka katika nafasi hiyo ya uongozi ni wazi walio chini yako watafuata mwenendo wako, lakini ukiwa mpigaji hata wa chini yako watapiga kwa ukubwa wao na ushindwe kuwakemea," alisema.

Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, Ismail Jussa, akitoa mada katika mafunzo hayo juu ya ahadi za ACT Wazalendo kwa Watanzania, alisema lengo kubwa ni kuhakikisha inajengwa Tanzania huru yenye kukua kiuchumi na kijamii.

Alisema haitoshi kukua kwa namba ya ukuaji wa uchumi usioendana na hali halisi ya maisha ya wananchi, na kwamba ni jukumu la viongozi waliopewa mamlaka kuhakikisha ukuaji huo, unawanufaisha wananchi wa kawaida.

"Idadi ya watu tulio nao ni utajiri tosha ikiwa tutatumia vizuri, ACT Wazalendo tuna Tanzania tunayoitaka nayo ni ile yenye kujali uhuru wa watu wake, haki na uwajibikaji kwa kuhakikisha wenye mamlaka wanawatumikia wananchi badala ya wananchi kuwatumikia wenye mamlaka" alisema Jussa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Lugha za matusi na ubaguzi ni sumu kwa ustawi wa nchi

**KWA** takriban miezi miwili sasa, kumekuwa na mjadala kuhusu suala la uwekezaji wa bandari kati ya Tanzania na serikali ya Dubai kupitia kampuni ya DP World. Mjadala huu umewagawa Watanzania kwa misingi ya itikadi za vyama vya siasa na wadau wengine wakiwamo viongozi wa dini, wanasheria na wachambuzi wa masuala ya kijamii na kiuchumi.

Makundi yanayohusika na mjadala huo, yaliibuka mara baada ya Bunge kuridhia azimio la makubaliano kati ya pande husika (IGA), yaani Tanzania na Dubai kwa nia ya kuleta ufanisi katika uendeshaji wa bandari nchini ili kuwe na tija na hatimaye kuongeza mapato yatokanayo na rasilimali hiyo.

Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikiongozwa na viongozi wake wakuu, mawaziri, wabunge na makada wakongwe, baada ya kuibuka mijadala hiyo, kimezunguka katika maeneo mbalimbali ya nchi kwa kile ilichosema ni kuwaelimisha wananchi umuhimu wa mpango huo wa kuendesha bandari kwa ufanisi kupitia DP World ya Dubai. Wakati CCM ikifanya hivyo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeanza kampeni yake maarufu kama +255 Katiba Mpya Okoa Bandari Zetu' kwa kile ilichodai ni kupinga mkataba huo.

Kadhalika lipo kundi la wanasheria ambalo limefungua kesi katika Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya likitaka tafsiri ya mkataba huo ambao limedai kuwa unakiuka sheria za nchi na kwamba ukuu wa nchi kuhusu ulinzi wa rasilimali zake umepokwa na kupewa nchi nyingine.

Hakuna jambo la ajabu katika jambo hilo kwa kuwa kuila upande unajaribu kutoa msimamo wake juu ya kile unachokiamini. Hiyo inatokana na ukweli kwamba Tanzania inaheshimu uhuru wa watu kujieleza, kutoa maoni ikiwa ni sehemu ya haki za binadamu kama zilivyoainishwa katika Katiba ya nchi.

Pamoja na ukweli huo, katika mijadala hiyo na mikutano inayoendelea kwenye majukwaa mbalimbali, kumekuwa na dalili za kuvukwa kwa mipaka ya uhuru huo kutokana na lugha zinazotumika ambazo asilani si za kiungwana. Ni lugha za matusi, kebehi na maudhi ambazo zinaweza kuamsha hisia mbaya miongoni mwa Watanzania na hata kufikia hatua ya kuibuka uhasama kwa misingi ya imani na itikadi.

Suala la mikataba linahusiana nini na suala la imani ya mtu kuwa ni wa dini fulani? Inakuwaje mtu anasimama jukwaani na kuporomosha matusi dhidi ya mtu mwingine bila kujali ni mkubwa kwake kiumri na anaongoza mamilioni ya Watanzania?

Sambamba na kugha hizo za matusi, pia kumekuwa na chembechembe za udini na ubaguzi kati ya imani moja na nyingine na upande mmoja dhidi ya mwingine wa pande za Muungano. Jambo hili pia linaweza kusababisha nyufa ndani ya Muungano hata kufikia watu kuhasimiana na hatimaye kuweka rehani tunu zetu za amani, umoja na mshikamano.


Watanzania hawajazoea masuala la kutukana na kukashfiana kwa misingi ya itikadi na imani ndiyo maana wamekuwa wakiungana na kushirikiana katika shida na raha bila kujali kabila, dini, rangi wala itikadi. Mambo haya yanapoibuka sasa wakati Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, uliozaa Tanzania, unakaribia kufikisha miaka 60, yanaleta ukakasi miongoni mwa Watanzania na wapenda amani kwa ujumla.

Ni vyema wanasiasa na wanasheria wanaposimama na kutoa kauli zao, wajenge hoja ambazo zitawafanya Watanzania wavutwe nazo badala ya kuibua matusi, kebehi na kejeli dhidi ya upande mwingine. Hoja lazima itolewe ili kushawishi watu wasio upande wa mtoa hoja na kama kuna ulazima ijibiwe kwa hoja zenye Mashiko na si vinginevyo.

Matusi ya aina mbalimbali, lugha za maudhi na ubaguzi kwa misingi ya imani na itikadi havina nafasi katika taifa la Tanzania na yeyote mwenye tabia hiyo, katu asivumiliwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Soko la Mawasiliano likumbukwe liendelee kustawi

Na Sabato Kasika

**WAMACHINGA** ni miongoni mwa wafanyabiashara muhimu, katika kukuza uchumi wao na wa nchi pia. Kwa umuhimu huo, serikali imekuwa ikiwajengea masoko wafanye shughuli zao katika mazingira mazuri.

Hatua ya kuwajengea masoko inatokana na kwamba wengi wao wamekuwa wakifanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi na mengine ya hatari kwa usalama wao yakiwamo ya barabarani na chini ya nyaya za umeme mkubwa.

Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo za serikali, baadhi ya wafanyabiashara hao wamekuwa wakihamishwa na kisha kurudi katika mazingira walioondolewa huku wakiwa na sababu mbalimbali.

Kwa mfano, soko la Mawasiliano lililopo Sinza Dar es Salaam, inaelezwa kuwa awali lilikuwa na wafanyabiashara 2,600, lakini kwa sasa wamebaki 964 baada ya kundi kubwa kuondoka na kurudi kule walikoondolewa.

Makamu Mwenyekiti wa soko hilo, Mussa Mbwani, anataja sababu ya baadhi ya wamachinga kuondoka kuwa ni mtindo wa kufanya biashara kwa mazoea unaoweza kusababisha waendelee kuhangaika huku na kule.

Kila mara katika masoko mbalimbali, wamekuwa wakilalamika kwamba hayana miundombinu yote, na kwamba yamejengwa mbali ambako wateja hawawezi kufika, lakini soko la Mawasiliano lina miundombinu yote.

**Kila mara katika masoko mbalimbali, wamekuwa wakilalamika kwamba hayana miundombinu yote, na kwamba yamejengwa mbali ambako wateja hawawezi kufika, lakini soko la Mawasiliano lina miundombinu yote.**

Soko hilo lina choo, maji na usafiri wa daladala kutoka maeneo mbalimbali ya jijini Dar es Salaam, lakini ajabu ni kwamba lina wafanyabiashara wachache, ninadhani ipo haja kwa Manispaa ya Ubungo kutafakari na kuchukua hatua za kuhakikisha linakuwa na wafanyabiashara wengi.

Huko walikokwenda sidhani kama ni salama na pia sidhani kama watakuwa wanalipa ushuru wa manispaa, kwani wengi wao ni wale wanapanga bidhaa kandokando ya barabara.

Lakini pia inaelezwa huko kandokando ya barabara, wamekuwa wakitozwa shilingi 1,000 wakiambiwa ni za ushuru, lakini zinaingia mifukoni Sh. 1,000 ambazo zinaingia katika mifuko ya wajanja wachache, kitendo ambacho kinaweza kuikosesha manspaa mapato.

Ushuru ambao mfanyabiashara analipa kila siku sokoni hapo, ni shilingi 500, hivyo waliokimbia kwenda kwingine, ninadhani ni sawa na kuruka majivu na kukanyaga moto, hivyo wangeamua kurudi.

Yawezekana wakawa wanauza bidhaa kwa wingi, hivyo hawaoni umuhimu wa kurudi sokoni hapo, lakini jambo la msingi ni kwamba masoko yamejengwa kwa ajili yao, wangeyatumia.

Masoko mengi ya Dra es es Salaam, yamekuwa yakifanyiwa maboresho ikiwamo kujenga vibanda kulingana na biashara ambayo machinga anafanya ili kuvutia wateja

Pamoja na jitihada hizo, baadhi ya wamachinga wamekuwa wagumu kuzijali, badala yake ni kukimbizana na serikali huku na kule ili mradi waendelee kubaki katika maeneo yasiyo rasmi.

Kwa ujumla, soko hilo liko eneo zuri, linafikika, ila shida moja tu ya baadhi ya wafanyabiashara kutojali kile ambacho kimefanywa kwa ajili ya, matokeo yao ni kukimbilia huku na kule badala ya kutulia sehemu moja.

Ninadhani, serikali bado ina kazi kubwa ya kuelimisha kundi hili kwa lengo la kulisaidia kujua haki na wajibu ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Tusizozanie posa mchumba akaghairi



**Pascal Mayalla**

UELIMISHAJI umma kuhusu DP World na bandari zetu umepamba moto. Kila mtu anaweza kuelimisha umma kuhusu hoja za kisheria? Hongera Chama Cha Mapinduzi (CCM) kujitolea kuelimisha umma. Ukweli utabaki kuwa wananchi hawahitaji hoja za kisheria bali matokeo chanya, bandari zetu ziboreke, zifanye kazi kwa ufanisi, Tanzania tupate manufaa na maendeleo endelevu.

Hii IGA ya DP World na bandari zetu, imetusaidia sana kujua mambo mengi, si tu imetusaidia kutuonyesha matundu kwenye paa la nyumba yetu kwa kutuonyesha panapovuja. Pia imetufungua macho kuona tuna wanasheria wa aina gani, wenye elimu gani na uwezo gani, ndiyo maana tunaingia mikataba ya ajabu ajabu, mingine ni mikataba ya ovyo. Tukija kushtuka, tunavunja hiyo mikataba, tunashtakiwa, tunashindwa, tunatozwa tuzo, tunajimwambafai kuwa hatulipi! Lakini mwisho wa siku, huwa tunalipa hizo tozo kimyakimya au tunalipishwa kwa nguvu kwa lazima baada ya mali zetu zikiwamo ndege kukamatwa.

Siku zote sheria ni fani yenye heshima kubwa katika jamii. Wanasheria ni watu nadhifu, wanavalia nadhifu, wanavaa majoho, wanaongea kwa mapozi, hivyo kuna wengi walitamani kuwa wanasheria lakini hawakuweza. Zamani kupata nafasi kusoma sheria ilikuwa kwa wale wanafunzi waliofaulu vizuri - wenye ufaulu wa daraja la kwanza pekee. Kwa maana hiyo, sheria ilikuwa fani ya vipanga tu.

Lakini sasa kutokana na kuongezeka kwa vyuo vikuu vya binafsi nchini, sasa kila mtu anaweza kusomea sheria. Si vipanga tu, hata vilaza nao sasa wana fursa ya kujiunga na vyuo vikuu wakasomea sheria, wanahitimu na kupata shahada ya sheria (LL.B) lakini uanasheria wao ni wa makaratasi, wa vyeti, yaani kusoma sheria. Kuhitimu na kupata cheti ni jambo moja, lakini uwezo wa kuifanya sheria ni jambo lingine.

Wanasheria hawa hawawezi kupenya Shule ya Sheria kwa Vitendo (LST) na kuwa mawakili! ila ni wazuri kwa kuongea. Wazuri kwa kufanya 'lobbying' na kujipenyeza kwenye nafasi mbalimbali. Usikute sasa baadhi ya hawa ndio wanasheria wetu tegemewa kwenye baadhi ya taasisi muhimu kama hiki kinachoendelea kwenye mjadala huu wa mkataba/ makubaliano ya IGA ya bandari.

Haya mambo ya kudogosha mambo makubwa, hayakuanza leo. Yalianza tangu enzi za Jei Kei na Eddo. Walikuwa vijana wawili marafiki. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, walikodi ndege moja pamoja, wakaenda Dodoma pamoja, wakachukua fomu za kugombea urais kupitia CCM pamoja, wakazitembeza pamoja kutafuta wadhamini na kuzirejesha pamoja. Watu wakawabatiza jina la Boys II Men, mmoja alionekana kama 'a boy' na mwingine 'a man'.

Baada ya Boys II Men kushindwa uteuzi wa mwaka 1995, ili kujiandaa kwa uchaguzi wa mwaka 2005 kundi la "mtandao" liliasisiwa likijumuisha watu mbalimbali, wakiwamo waandishi wa habari na vyombo vya habari, kazi yao kubwa ikiwa kuhakikisha 'a boy' ndiye anapenya katika uteuzi wa urais. Kweli 'The Boy' akashinda urais, akaunda serikali, huku 'the Man' akifanywa kiranja Mkuu. Baadaye Boys II Men wakafarakana, ikamlazimu Eddo kuachia ngazi.

Kutokana na 'the Boy' kumaliza muda wake wa uongozi wa miaka 10, mwaka 2015 kukatokea harakati na vuta nikuvute za kugombea urais. Kuna watu wakajiona kama 'the Boy' ameweza kuwa rais, basi kila mtu anaweza kushika nafasi hiyo ya juu kabisa katika uongozi wa nchi, wakajitokeza wagombea 62!

Hiki kinachoendelea kwenye mjadala wa IGA ya DP World na bandari zetu, kumeidogosha sana fani ya sheria. Sasa kila mtu anajiona ni mwanasheria. Hali hiyo imefanya wanasheria waonekane si watu muhimu. Mtu yeyote anaweza kuwa mwanasheria na si kila mwanasheria aliyesomea sheria ni mwanasheria. Wengine ni wanasheria wa makaratasi tu, naendelea kusisitiza.

Hoja za kisheria zilizoibuliwa kuhusu hii IGA zijibiwe kisheria na si kisiasa. Kwa vile na mimi ni mwanahabari mwanasheria, najitolea kuelimisha umma kuhusu IGA na HGA. Kwa lugha rahisi, IGA ni kama barua ya posa tuu kwa DPW kumposa binti yetu Bandari.

Uhusiano wa wawili hawa ulianza toka Februari, 2022 wakati wa Expo Dubai. Mwarabu wa Dubai, alimwona binti Bandari Dar es Salaam, kampenda. Akamwalika mzazi wa binti kutembelea Dubai wakati wa Expo Dubai, ndipo DPW akatangaza nia ya kumposa binti Bandari Dar es Salama.

Kwa nia njema makubaliano ya awali (MoU) kati ya Bandari na DPW yakatiwa saini Dubai huku mzazi akishuhudia. Makubaliano hayo ni ni kumruhusu DPW kuleta barua ya posa. Oktoba, DP World katua nchini na mshenga wake kuleta barua ya posa, ndiyo hii IGA.

Mzazi wa binti ni Mama Harusi akamruhusu mjomba mtu, Profesa kuipokea barua hiyo ya posa, ikapokewa Oktoba, 2022. Mzazi wa binti Bandari, akaipeleka posa kwenye kikao cha wanafamilia, kuomba ridhaa ya posa ikubaliwe binti Bandari aposwe na DPW. Kikao cha familia, kikaridhia, ndicho kile kikao cha Bunge kuridhia IGA.

Baada ya posa kukubaliwa yaani baada ya ile IGA kuridhiwa sasa ndio mahari ya binti yetu inapangwa ambayo itakuwa ni HGA. Kiafrika kitendo cha binti kuposwa ni heshima kubwa. Wajomba msipigie kelele barua ya posa, mchumba asije kughairi. Tutulie, tupange mahari ya maana, binti Bandari aolewe!

**Wasalaam,**
**Paskali 0754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kama vipi chupa ya chai ivunjwe tutumie mabakuli



**Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)**

KUNA hadithi ya mtoto mharibifu, aliyekuwa na tabia ya kuharibu vifaa nyumbani, kiasi cha kumfanya mama yake kuwa kama kichaa akimlinda kila wakati.

Hali hiyo ilimfanya mtoto kuishi kwa wasiwasi, huku akipendelea sana kuwa karibu na chupa ya chai ambayo ilihusika katika kumtunzia uji na maziwa na kila mara akihatarisha kuivunja.

Mama naye aliingiwa na wasiwasi kuwa endapo chupa hiyo itavunjika atafanya nini wakati hali yake kiuchumi ilikuwa duni, hivyo asingemudu kununua nyingine.

Mara zote akawa mtu wa kukemea, akijua ikitokea akakaa mbali huyu mwanawe, bila shaka maisha ya chupa ile yatakuwa shakani na hatapata nyingine.

Kwa kuwa sasa ilionekana kero kwa mtoto yule, siku moja akapata wazo la kumaliza wasiwasi aliokuwa nao, nalo likawa la kuivunjilia mbali ili isiwapo tena na kelele za mama ziishe.

Kweli, siku moja alipoamka na kupata kifungua kinywa chake kama kawaida kupitia chupa ile, mama aliaga kwenda sokoni kununua mahitaji ndipo mtoto akaona huo ndio ulikuwa wakati mwafaka.

Aliivunjilia mbali chupa ile na mama aliporudi akakutana na vipande vipande na alipohoji kwa hasira, mwanawe alilia na kumwambia hakuwa na jinsi, ila kuondokana na udhia ule.

Kuanzia siku hiyo, nyumba ikawa ya amani licha ya sasa uji, chai na maziwa kuhifadhiwa na kunywewa kwenye vikombe na mabakuli na hatimaye kila kitu kikasahaulika na maisha yakaendelea.

Nimemsikia takriban mara tatu, nne hivi, Mama, Chifu Hangaya, Rais Samia Suluhu Hassan, akililia amani na utulivu wa nchi na hasa kuchelea Watanzania kugawanyika kutokana na jambo, mtu au kikundi cha watu.

Kilio chake kinapaa zaidi kutokana na muktadha wa kelele za mkataba wa ushirikiano wa serikali za Tanzania na Dubai, kuhusu uwekezaji kwenye bandari za Tanzania.

Anaona kama tunavyoona sisi kwamba kuna mgawanyiko unaolemea Watanzania wanaojadili mkataba huo katika nyanja na medani mbalimbali, wakiwamo wanaopinga mkataba, wanaounga mkono na wasio na msimamo.

Kuna mgawanyiko wa kimsimamo na kimawazo baina ya wanasiasa, wataalamu, wanahabari, viongozi wa dini na wanasheria, kila upande ukivutia ngozi kwake kwa sababu dhahiri na fiche.

Jina maarufu linalobamba miongoni mwa ndimi za jamii ya Watanzania ni DP World, kampuni inayopigiwa upatu na kupingwa kuwekeza katika bandari nchini. Uzuri ni kwamba makundi yote hayo hakuna linalopinga uwekezaji.

Bali katika makundi hayo, kuna wanaohoji mkataba na vipengele vyake, lakini wapo wasiotaka kujishughulisha na mkataba ila DP World apewe tu hata kama ni bandari zote, zikiwamo za mabwawani.

Bila shaka Chifu Hangaya pia ametishwa na jinsi matusi yanavyorushwa ovyo na watu bila kujali rika, utadhani wamevutishwa bangi. Mdogo anamtukana mkubwa bila kujali na mkubwa anamwaga mitusi bila aibu wala hofu!

Kwa hali hiyo, mama yeyote mwenye dhamana ya kuangalia wanawe akitaka waishi pamoja kwa mshikamano thabiti, lazima atasimama na kukemea hali hiyo isiyo na siha, kwa mustakabali mwema wa familia, ukoo na taifa kwa ujumla.

Lakini ili kuondokana na sintofahamu hiyo, Watanzania wachache miongoni mwetu, wakaona ni bora kwenda mahakamani kuangalia ni nini hasa kilichomo kwenye mkataba na kama kinaweza kufafanuliwa na kueleweka ili kuondoa mtanziko uliopo.

Ni bora Mahakama ikavunja chupa hii, ili tuondokane na taharuki iliyopo hivi sasa kwa sababu hakuliki, hakulaliki hivi sasa kisa ni mkataba-chupa iliyoko mikononi mwa mtoto.

Watu wanataka kujua; je, uwekezaji huu unaungwa mkono na kila Mtanzania? Kutiwa saini, kuwasilishwa bungeni na kuridhiwa kwake kulishirikisha Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Rasilimali na Maliasili?

Je, kulishirikisha Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti hasi katika mikataba inayohusu Rasilimali na Maliasili za Nchi? Umma uliarifiwa na kupewa muda mwafaka kushiriki na kutoa maoni yake?

Je, zile ibara 14 za mkataba wenyewe zinakiuka ibara zile tatu za Katiba ya Tanzania? Na ibara mbili za mkataba zinakiuka kile kifungu kimoja cha Sheria ya Mikataba ya Tanzania?

Kama haitoshi, je, makubaliano (IGA) kati ya Tanzania na Dubai yalifuata taratibu za kisheria, kuchagua njia ya ununuzi ambayo iko chini ya kifungu cha 64 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma? Na je, makubaliano hayo ni mkataba na walioshiriki kuyasaini walikuwa na nguvu ya kisheria?

Majibu ya je, je, je hizi, yatapatikana mahakamani na ndipo sasa Watanzania wataona nini kinafaa. Vinginevyo Mama avunje tu chupa ya chai ili tuendelee na maisha ya kunywea kwenye vikombe na mabakuli.

**Alamsiki!**

# Nchemba: Uswisi ina msaada mkubwa uchumi wa Tanzania

Na Halfani Chusi

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema Serikali ya Uswisi, imekuwa msaada mkubwa katika kukuza uchumi wa Tanzania kupitia uwekezaji walioufanya kwenye sekta mbalimbali ikiwamo biashara na uwekezaji.

Nchemba aliyasema hayo juzi kwenye sherehe ya maadhimisho ya pili ya miaka 732 ya Shirikisho la Uswisi, yaliyofanyika nyumbani kwa Balozi wa Uswisi, Osterbay mkoani Dar es Salaam.

Alisema kwa miaka mingi serikali ya Uswisi imekuwa mdau mkubwa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwamo, kilimo, elimu, utalii, biashara, uwekezaji na ustawi wa jamii.

"Tunawapongeza pia, kwa kuendelea kutuunga mkono kwenye maeneo mengine kama mafuta na gesi, usafiri wa anga, na maeneo mengine ya kiuchumi," alisema.

Dk. Nchemba alisema urafiki kati ya nchi hizo unaendelea kukua siku hadi siku na kwamba kwa sasa wanaangalia namna ya kuufanya kuwa imara na endelevu.

Kiongozi huyo alisema miaka ya hivi karibuni Uswisi ilitajwa kuwa ni miongoni mwa nchi zinazoisaidia Tanzania kwenye nyanja mbalimbali.

"Kupitia huu urafiki, tutaendelea kuomba msaada kwao, ili kutimiza ile adhma ya kuwa Tanzania ya viwanda," alisema Nchemba.

Balozi wa Uswisi Nchini, Didier Chassot, alisema serikali yao imekuwa ikitoa msaada kwenye miradi mingi ya maendeleo tangu mwanzoni mwa miaka ya 1960 na kwamba nchi hizo zina historia ndefu ya ushirikiano wenye manufaa.

# Kinana abeba dhamana kilio bei ya pamba

**Na Maulid Mmbaga,** ITILIMA

KILIO cha wakulima wa pamba kuhusu kushusha kwa bei ya zao hilo na kuchangia kuendelea kuwa maskini kimepokewa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuahidi kuzungumza na serikali kuona namna ya kutatua tatizo hilo.

Jana, wilayani Itilima mkoani Simiyu, wakulima waliwasilisha kilio chao kuhusu kushuka kwa bei ya pamba na kuchangia kuendelea kutafunwa na umaskini kauli ambayo Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, aliahidi kuzungumza na serikali kuona namna ya kuitatua.

Akijibu swali la wakulima katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Laini, Kinana alisema changamoto hiyo inapaswa kutatuliwa na serikali.

Kinana aliahidi kuliwasilisha ngazi za juu ili kuona namna ya kujenga viwanda vya ndani vya kuchakata zao hilo kwa kutengeneza nyuzi na nguo na kunusuru bei ambayo inashuka kila msimu.

Malalamiko ya wananchi yanalenga zao hilo kuwa na bei elekezi ili kuondokana na changamoto ya kila msimu pamba kuuzwa bei ya chini na hata inapouzwa malipo huwa nusunusu na kushusha thamani yake huku gharama za uzalishaji zikipaa.

Akizungumza na wananchi Kinana alisema: "Jambo hili si la kwenu wakulima ni la serikali na mimi nalichukua kwenda kuonana na wakubwa kuwaambia, wakulima wanalima bei inashuka kwa sababu hakuna viwanda nchini."

Alisema serikali inapaswa kujitahidi kujenga viwanda vya kuchakata zao hilo ikiwamo kutengeneza nyuzi na nguo ili wakulima wasitegemee soko la nje ya nchi pekee katika kuuza.

Pia, alisema kuendelea kupeleka pamba kwenye soko la nje ya nchi ni wazi kwamba bei ya zao hilo itaendelea kuwa ya chini kwa kuwa wao wanapanga wanunue malighafi hiyo kwa bei ya chini. "Jibu lingine la bei nzuri ya zao hili kila mkulima anatakiwa kulima kilimo cha kisasa, mfano nimeona Singida kuna mkulima mmoja anapata kilo 1,000 wakati Mkuu wa Mkoa wa Simiyu aliyelima karibia heka moja alipata kilo 500.

"Wewe unayelima hapa kwa utaratibu wako heka moja unapata kilo 150 hamuwezi kufanana kimapato. Sasa ni kazi ya serikali kuwaleta wataalamu wawafundishe wananchi walime kilimo cha kisasa," alisema.

Kinana alisema kutokana na changamoto hiyo anakusudia kuonana na Waziri wa Kilimo ili kuzungumza naye kuhusu kusuasua kwa malipo ya wakulima baada ya kuuza zao hilo.

"Kuendelea kulipwa nusunusu kila wanapouza pamba yao linafanya zao linakosa thamani na kuendelea kuwasumbua wakulima wanaotumia gharama kubwa katika uendeshaji wa zao hili," alisema Kinana.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba (TCB), Marko Mtunga, alisema asilimia 80 ya pamba inayozalishwa inapelekwa nje ya nchi ndiyo maana hakuna bei elekezi inayojulikana.

"Ni vigumu kwa wakulima wanaokwenda shambani mwezi Desemba kufahamu bei na ili tuweze kuwaeleza bei, tunapaswa kuwa na mfuko wa kinga ya bei. Ukiwa na fedha kwenye mfuko bei, ikishuka mfuko unatoa fedha unajazia," alisema Mtunga.

Hata hivyo, alisema tayari serikali imeanza kuchukua hatua na katika mwaka huu wa fedha, imeanzisha mfuko wa kilimo ambao, moja ya kazi yake ni kudhibiti soko na kuwafanya wakulima kuwa na uhakika.

"Ni ukweli mwaka huu bei imeshuka. Mwaka jana wapo waliouza kwa bei ya Sh. 2,000 kwa kilo moja wakati bei elekezi ikiwa Sh. 1,560 na wakati tunapanga bei hiyo msimu uliopita katika soko la dunia bei zilikuwa kubwa," alisema Mtunga.

Mkulima Eliya Ngenda alitaja changamoto nyingine wanayokutana nayo ni pembejeo.

"Dawa wanazoletewa kwa ajili ya zao hili zimekuwa chini ya kiwango, tunapulizia ndani ya muda mfupi magonjwa kama funza wanaendelea kushambulia mazao," alisema Ngenda.

Mkulima Sagata John alisema: "Serikali imekuwa kimya na chama hakijaja kutoa elimu bei imeshuka na tunapaswa kufanya nini? Wametuacha tukipambana na madalali kila kukicha na hakuna wakutusaidia."



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo (wa tatu kulia), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa mmoja wa wagonjwa waliolazwa katika kituo cha Afya cha Naipanga, kama sehemu ya maadhimisho ya siku ya mashujaa hivi karibuni. Wa (pili kulia) ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Mhandisi Chionda Kawawa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TenMet yaomba nyongeza ya ruzuku shule za msingi

**Na Mary Geofrey**

MTANDAO wa Elimu nchini (TenMet), umeishauri serikali kuongeza ruzuku ya wanafunzi wa shule za msingi kuwa zaidi ya 6,000 kwa mwanafunzi mmoja katika bajeti ya kutoa elimu bure.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Programu wa TenMet, Martha Makale, alisema wanaishauri serikali isimamie uwajibikaji, utendaji wa viongozi na watoa huduma katika sekta ya elimu na utawala.

Pia iboreshe upatikanaji wa walimu, kuwagawa kwa uwiano sawa kwa kuzingatia jinsia mahitaji maalum na mpangilio wa jiografia.

Ushauri huo aliutoa wakati akizungumzia kuhusu taarifa ya uwezeshaji jamii katika kusimamia serikali za mitaa na watoa huduma katika kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora katika shule za umma katika mradi uliotekelezwa kwenye halmashauri 10.

Makale alisema mradi huo ambao umehusisha wadau wa ngazi ya jamii zikiwamo kamati za shule, viongozi wa vijiji, halmashauri, taasisi za sekta binafsi na watunga sera, umebaini kuwa, ruzuku zinazotolewa kwa shule za msingi zipo chini ya kiwango cha 6,000 kwa kila mwanafunzi.

Alisema asasi ya TARUCODEFU iliyoko Kibiti, mkoani Pwani, ilibaini ruzuku iliyofika shuleni ni 5,400 hadi 5,600 kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 badala ya 6,000, hivyo wanataka iongezwe ili kukidhi mahitaji.

Alitaja jambo lingine ni wazazi kutokuwa na taarifa sahihi na kutoshirikishwa katika vipaumbele vya shule, ikiwa ni pamoja na mipango na mchakato mzima wa makadirio ya mapato na matumizi.

Mshauri wa TenMet, Japhet Makongo, alisema wamebaini kukosekana kwa miundombinu sahihi ya kufundishia ikiwamo madarasa, vyoo, nyumba za walimu, viwanja vya michezo na vifaa.

"Katika shule zote zilizofikiwa na mradi wa SAM/PETS, kulikuwapo na msongamano wa wanafunzi darasani hususani kwa madarasa ya awali katika vijiji vya mbali au vilivyoko pembezoni wilayani Kalambo, Nsimbo, Mvuha/Morogoro, Pangani, Nachingwea na Kibiti," alisema.

Alisema pia, kumekuwapo na ndoa za utoto na mimba kwa wasichana na unyanyasaji wa kijinsia ulioshuhudiwa katika wilaya za Chamwino, Kalambo, Nsimba, Pangani na Nachongwea.

"Tatizo linachangiwa na wenye mamlaka kushindwa kuwajibika ipasavyo," alisema.

Meneja Umegaji na Rasilimali, William Chacha, alishauri kuwapo kwa uwajibikaji na ufuatiliaji wa Rasilimali za Umma (SAM), unatengeneza mfumo wa kuhamasisha jamii kushiriki moja kwa moja katika kuibua mawazo mbalimbali, kupata taarifa na kusimamia uwajibikaji.

"Hii inaonyesha kuwapo kwa umuhimu wa mabadiliko ya mawasiliano kati ya serikali na jamii na serikali, kuzingatia misingi ya utawala bora," alisema Chacha.

Aliongeza kuwa SAM umewezesha kuwapo kwa mabadiliko katika kujenga uhusiano kati ya jamii na serikali, hivyo kuwajengea hali ya kujiamini na kuwa tayari kufuatilia watoa huduma.

# MAISHA

JULAI 30, 2023

**Nipashe**

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*

Ukurasa 14




## VILEJA VYA TAMBI

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



ISHI NYUMBA INAYOKUPA FURAHA




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# KOTI LINAKUPA HADHI

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| O | ■ | J | E | M | B | E |
| N | ■ | ■ | ■ | K | ■ | N |
| G | ■ | F | A | O | ■ | D |
| O | V | U | ■ | S | I | E |
| Z | ■ | M | O | I | ■ | L |
| W | ■ | B | ■ | ■ | ■ | E |
| A | M | A | N | A | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

ARA, DAU, MBU, TIN, OTANA, FUNDA, NINDU, TAMKA, AMBULIA, MAKALIO

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 4 | 2 | 3 | |
| 1 | | 2 | 4 |
| | | | |

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO wa miaka sita alimuuliza babake:

MTOTO: Baba, eti sisi wanadamu tulikuja vipi duniani?

BABA: Mungu alimuumba Nabii Adam na Hawa. Kisha wao wakaanza kuzaa watoto na watoto wakazaa mpaka tukazaliwa sisi. (Mtoto hakuri dhika akamfuta mamake)

MTOTO: Mama, eti sisi wanadamu tulikuja vipi duniani?

MAMA: Wanasayansi wamesema sisi tulitokana na manyani baadae tukawa binadamu. (Mtoto akarudi kwa baba)

MTOTO: Baba mbona mama anasema sisi tulikuwa manyani mwanzo?Au wanidanganya?

BABA: Mwanangu, mimi nimekuelezea kuhusu ukoo wetu. Mamako amekuelezea kuhusu ukoo wao.

**SWALI**

Samaki aina ya Pweza ana mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Anayopaswa kufanya mwanamume anapokuwa hai

KARIBU tena msomaji wangu tumalizie sehemu ya mwisho ya mfululizo wa makala zetu kuhusu mke, mume na wakwe katika maisha ya ndoa. Wiki iliyopita tuliona mambo mbalimbali anayopaswa kufanya mke awapo kwenye ndoa.

Leo nimulike mambo anayopaswa kufanya mwanamume anapokuwa hai ili kuiepushia ugumu familia yake siku za usoni. Kila mwanamume mwenye hekima huhudumia familia yake kwa ajili ya maisha ya hapo baadaye, iwe yuko hai au la.

Yampasa mtu ajiulize je, ikitokea umeondoka duniani nini kitatokea kwa mke na watoto wako? Hatuombei lakini Maisha Ndivyo Yalivyo kwamba kuondoka hapa duniani ni ratiba ya Mungu vile impendezavyo.

Je, wataishi maisha bora au watachanganyikiwa? Je, ni vitu gani umeviandaa au bado wewe unaamini kuwa bado ni mdogo sana kufa mapema. Kumbuka watu kwenye umri mdogo wanaweza kufa kwa sababu ambazo Mungu peke yake anazijua.

Fanya maandalizi ya siku za usoni kwa ajili ya mke na wanao. Uchunguzi ambao umefanyika umeonyesha kuwa asilimia 90 ya wanawake na watoto wao hupata mateso ya ajabu sana pale waume zao wanapofariki dunia.

Ndugu zako wanaojifanya wanapenda familia yako na mkeo, huwageuka pale wanapojua haupo tena kusimama na kuwatetea. Nikutajie hapa baadhi ya mambo wanayopitia wajane pamoja na watoto wao.

Kwanza, huwa wanatengwa. Hakuna mtu anayetaka kujumuika nao. Pili, huwa wanadhalilishwa. Wengine hulazimishwa kufanya mambo ambayo ni kinyume cha utu wa mtu. Huwa wanakuwa wapweke, wenye hofu na shaka muda wote.

Wengine husingiziwa wameua waume zao. Mfano, kipindi cha kuuguza, hata kama mama amejitahidi vipi kumhudumia, bado ataonekana msaliti.

Wengine hunyang'anywa mali zao na ndugu wa mwanaume na kuwaacha kuhudumia watoto wao peke yao. Wanapoteza heshima za waume zao waliokufa kwa kulazimishwa kuolewa na ndugu upande wa waume zao.

Pia husingiziwa uchawi. Wajane huonekana kama mzigo, hivyo watu huwakimbia na kukaa mbali nao. Kama watoto walikuwa wanasoma, wengine huacha hata shule kwa kushindwa kulipa ada. Hakuna ndugu anayetoa msaada wowote.

Wajane huonekana kama watu wasiofaa katika jamii nyingi. Inakuwa mbaya zaidi kama wakati wa uhai, mwanamume alikuwa hana ushirikiano na ndugu au jamaa zake.

Sasa, ufanyeje ili uhakikishe mke na watoto wanabaki salama wakati wewe haupo? Kwanza, mshukuru Mungu kwamba bado uko hai, bado unaweza kufanya kitu. Na kama unaweza basi usipoteze muda, fanya haraka.

Hakikisha kuwa mrithi wa mali zako anakuwa mkeo. Usithubutu kumfanya mama yako, kaka, dada, binamu na kadhalika kuwa mrithi wako, kama hutaki familia yako kukosa mali zote, ulizotaabikia miaka mingi na kuwafanya waendelee kutaabika!

Hakikisha umeandikisha nyaraka zako za urithi na kumwandika mke wako mpenzi kama msimamizi wa mali zako zote. Hilo ni jambo bora na la busara kuliko yote unayoweza kufanya.

Nunua nyumba nyingi, magari na uandikishe kwa majina yenu wawili, au zaidi kwa jina lake au majina ya watoto wenu. Mpende mke wako na usikubali ndugu zako wawatenganishe.

Usije ukathubutu kumsema mke wako vibaya kwa ndugu zako. Ni wanaume wachanga wanaoweza kufanya hivyo! Mkatie mkeo na watoto bima ya maisha yao.

Mke wako anapaswa kufahamu miradi yako yote. Fungueni akaunti ya pamoja wewe na mke wako. Mweke mke wako wa kwanza, katika jinsi unavyowahudumia na jinsi atakavyohudumiwa na ndugu zako.

Omba kwa ajili ya maisha marefu na yenye mafanikio. Fanyeni maombi ya pamoja kusambaratisha na kubatilisha kila mipango ya adui juu ya familia yenu. Kuwa mwaminifu kwa mkeo. Usipofanya hivyo utakuwa umejitafutia kufa mapema pale utakapokuwa na wanawake wengine nje ya ndoa (makahaba, nyumba ndogo).

Hakikisha mke wako anafanya kazi ili umjengee msingi mzuri wa kujisimamia pale utakapokuwa haupo duniani. Usimlazimishe awe mama wa nyumbani kwani atateseka sana utakapokuwa haupo.

Wapeleke watoto wako shuleni, wape elimu bora ili baadaye wawe na uwezo wa kujitegemea. Waongoze watoto kumjua Mungu. Huu ni urithi mkubwa utakaokuwa umewaachia watoto wako.

Mfanye Mungu awe kiongozi wa nyumba yenu, mkabidhini maisha yenu yote ya siku za usoni.

***Je, una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Watawala, NGO ni mkono wa pili wa serikali

WAKATI nakua, nilikuwa nikimsikia mama yangu na hata wanajamii wengine wanaotuzunguka wakitumia misemo ya zaidi ya aina nne, inayosisitiza juu ya huruma, upendo na kukirimiana kati ya mdogo na mkubwa.

Moja ya misemo ambayo naikumbuka hadi leo ni huu unaosema "hicho chakula mbakizieni mdogo wenu."

Kipindi fulani, mama yangu alikuwa akiniagiza, mkifua nguo zenu msisahau na za mdogo wenu. Mara utamsikia akikazia jambo hilo hilo, chezeni michezo mizuri msimuumize mdogo wenu.

Au tulipokuwa tumetoka zetu kucheza mtaani na watoto wengine, mama anatuuliza mie na dada yangu, mmerudi wenyewe mdogo wenu yuko wapi?

Jamii iliyostaarabika duniani kote inajua, asasi za kiraia au mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) ni mkono wa pili wa serikali. Kwamba, kila wanachokifanya, ni kile ambacho serikali inapaswa kukifanya kuhudumia watu wake, ndiyo ukweli ulivyo!

Lakini sera na taratibu zinazosimamia utozaji kodi kwa asasi za kiraia, bado si rafiki kwa wanaoanzisha na kuendesha mashirika hayo yasiyo ya kiserikali.

Hakuna shaka kwamba asasi za kiraia zinawajibika kulipa kodi na kuwasilisha marejesho (returns0 kwa mujibu wa Sheria Namba 24 ya Mwaka 2002 inayounda asasi hizo.

Kiuhalisia, ritani ya kodi ni hati inayowasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambayo inaonyesha mapato, gharama na taarifa zingine zinazohusiana na mwenendo wa shughuli za kiuchumi kama inavyotakiwa kisheria.

Hivi sasa, ritani ya kodi inahitajika kuwasilishwa kwa njia ya kielektroniki (e - filling) kwa madhumuni ya urahisi.

Ni kweli kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali yamesamehewa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye uingizaji au/ ununuzi wa bidhaa au huduma kwa shirika lenye makubaliano na serikali, kwa ajili ya mradi unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali.

Yote hayo yanafanyika ikiwa makubaliano hayo yameainishwa kuwa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa au huduma.

Wiki hii, kuliripotiwa kilio cha tozo ya kodi ya mwaka ya asilimia 30 inayotokana na mavuno ya mapato ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) kwamba inawaumiza kwa vile wao hawafanyi biashara zaidi ya kutoa huduma.

Mratibu wa Taifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Wakili Onesmo Olengurumwa, amenukuliwa akisema ziko kodi za kawaida ambazo wanaweza wakalipa, lakini zingine ambazo wanapigwa, kwa mfano kodi ya mwaka ya asilimia 30 ya mapato, wao hawana mapato.

Olengurumwa anasema: "Sisi tuna ruzuku na ruzuku si ya mtu binafsi ni ya kuhudumia. Sasa ruzuku yangu ambayo inatumika mwaka kesho, ukipiga asilimia 30 maana yake umeenda kutumia hela ya miradi.

"Ndiyo maana tumeona tukae vizuri na ndugu zetu wa TRA pamoja na serikali ili tuweze kuona ni namna gani tutaboresha sheria za kodi zikatutambua sisi kama walipa kodi, ambao tunafanya kazi za kijamii. Tubakie tu na zile kodi za msingi kama ukilipa mishahara lazima ukatwe kodi."

Maana yake ni kwamba kilio hiki cha asasi za kiraia kimezagaa kila kona ya nchi. Wanalia! na ombi lao kubwa ni kupata misamaha ya kodi hiyo inayolalamikiwa.

Kwa mfano, Msajili Msaidizi wa NGO Mkoa wa Kilimanjaro, Jesca Nyaki, amenukuliwa akisema mkoa huo wenye jumla ya mashirika yasiyo ya kiserikali 443, yaliyosajiliwa chini ya Sheria ya Uratibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Namba 24 ya Mwaka 2002, ni 110 pekee ambayo yamewasilisha taarifa zao na miradi yanayoitekeleza, lakini 333 yameficha taarifa zao na hayajulikani yanafanya nini.


Mashirika yaliyojisalimisha mwaka 2022, ni yale yanayotekeleza shughuli mbalimbali zikiwamo shughuli za afya, elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia na elimu ya ujasiriamali.

Mengine ni yale ya ukuzaji wa uchumi, utunzaji wa mazingira na wako wadau ambao wanatoa huduma za msaada wa kisheria na kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwa kuanzisha vituo vya kulea watoto.

Tukiangalia kwa mwaka 2022, yametekeleza shughuli mbalimbali ambazo zina takribani thamani ya Sh. bilioni 6.1. Hawa wapewe maua yao.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kwa mamka uliyo nayo na nafasi uliyopewa ya kumshauri Rais Samia Suluhu Hassan katika masuala ya kodi, itazame upya tozo ya kodi ya asilimia 30 wanayotozwa NGO.

• ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***





Njia za kumshtukiza mpenzi wako kama unataka kumchumbia ziko nyingi. Pichani ni baadhi ya picha zinazoonyesha jinsi ya kumwomba uchumba kwa namna ya kipekee.



# MITINDO









# KOTI LINAKUPA HADHI

JUKUMU la kuteua nguo gani za kuvaa, linabaki kwako binafsi ili kuondoa malalamiko.

Hata hivyo, uchaguzi ni lazima kuwa na uelewa mpana kuhakikisha unapata nguo bora na maridadi.

Kwa ujumla kabla ya kupata aina yoyote ya nguo ni muhimu kuzingatia mambo mengi.

Tuangalie namna unavyoweza kufanya chaguo sahihi la kupata koti safi.

Kwanza zingatia mtindo wako wa vazi. Hapa ndipo ladha inachukua jukumu la msingi wakati wa kuchagua kati ya aina tofauti za koti.

Hivi sasa kuna aina anuwai ya koti za wanaume kwenye soko.

Haitofautiani tu kwa sura, bali pia kwa mtindo. Koti imeundwa kwa nyenzo tofauti ambayo inafanya utafutaji uwe rahisi zaidi.

Pili, rangi hutumika kama hitaji kuu kulingana na mwonekano wako.

Mfano ya makoti ya kisasa kwa wanaume inamfanya aonekane maridadi.

Vazi hili linachanganya rangi na mitindo ya suruali kuwa nguo rasmi.

Aidha, Blazer kwa wanaume ni kitu cha kupendeza zaidi, inatumika ikiwa maeneo ya kazini au kwenda matembezi.

Kumbuka kuwa koti inaleta tofauti ambayo inampa mtu mwonekano mzuri.

## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# Utafanyaje kuondoa kikwapa?

KUNUKA kikwapa ni tatizo kubwa katika mwili wa binadamu. Tatizo hili husababishwa na bakteria wanaovutiwa na jasho au unyevunyevu chini ya kwapa.

Kuna njia nyingi ambazo watu wengi huzitumia ili kwapa liwe na harufu nzuri, kavu na safi.

Wengine hutumia njia za kisasa ambazo ni pamoja na kupaka doodoranti au pafyumu zinazosaidia kuondoa harufu mbaya mwilini.



Lakini kama hiyo haitoshi, kuna njia za kisasa zinazoweza kuzuia harufu ya kwapa.

Njia za asili

Kupaka kipande cha limao kwenye kwapa na kuacha lipate hewa safi ili kuua vijidudu na kutoa tezi za jasho kuondoa harufu mbaya.

Kuvaa nguo safi zenye nyuzinyuzi za asili kama pamba, hariri na sufi zitasaidia kufyonza unyevu na kuliacha kwapa lako kuwa kavu, safi na bila harufu mbaya.

Kuoga kila siku na kusafisha nguo kwa maji safi kunasaidia kuua bakteria na ambao husababisha harufu mbaya.

Pia kunywa maji mengi kila siku kunakusaidia kutoa sumu mwilini na hivyo kupunguza harufu mbaya ya kwapa.

Njia nyingine inayoshauriwa ni kuhakikisha kuwa unaosha kwapa mara kwa mara kwa kutumia sabuni zenye dawa kemikali ya medicated.

Mambo ya kuzingatia

Aidha, kupunguza kula chakula chenye viungo vingi hasa vitunguu. Inasemekana kuwa kula vitunguu vingi kunachangia mwili kutoa harufu kali.

Pia inashauriwa kuwa baada ya kuoga jifute kwa taulo au kitambaa safi na usiache unyevu unyevu ambao huwavutia bakteria kukua katika maeneo yaliyojificha.

Mbinu nyingine ni kujitahidi kunyoa nywele za kwapa mara kwa mara na kuepuka kukaa sehemu zenye joto kupita kiasi kwa muda mrefu.



## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Vileja vya tambi

VILEJA ni aina ya vitafunwa ambavyo mara nyingi familia hupendelea kula lakini kupika wengi hawafahamu.

**Mahitaji**

Tambi nyembamba mifuko miwili, siagi vijiko vya supu vinne, maziwa ya sona 300Ml

zabibu kavu kikombe kimoja, arki (vannila) Kijiko cha supu kimoja,

**Jinsi ya kupika**

Weka karai au sufuria kwenye moto kiasi tia siagi, weka tambi uzikaange usiachie mkoni mpaka ziwe rangi ya dhahabu.

Kisha weka zabibu huku unakoroga, weka maziwa na huku unakoroga usiachie mkono na weka arki.

Ipua karai, tumia kijiko cha chai kwa kuchotea na utie kwenye kikombe cha kahawa nusu usikijaze.

Kipindue kwenye sahani utoe kileja na acha kwa dakika 10 vitakuwa tayari kwa kuliwa.







MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# ISHI NYUMBA INAYOKUPA FURAHA

MIONGONI mwa maeneo ambayo huwa ni faraja na ya kupumzisha akili baada ya shughuli nyingi ni nyumbani.

Nyumbani ndipo palipo na mkusanyiko wa maisha, kumbukumbu na upendo kwa asilimia kubwa ya watu.

Binadamu kila mmoja hujishughulisha na mambo mbalimbali lengo likiwa ni kujitafutia riziki na kuhakikisha mkono unakwenda kinywani na mambo mengine ya kifamilia yanakwenda sawa.

Pamoja na kujishughulisha huko, mwisho wa siku lazima arejee nyumbani kujipumzisha bila kujali umbali wake.

Hivyo basi, kwa vyovyote vile lazima uhakikishe nyumbani panakuwa mahali sahihi, panapokupa furaha, amani na utulivu.

Si tu kwa utulivu, ni muhimu kuzingatia kwamba nyumba hiyo ya kuishi ipo eneo ambalo halitakusababishia karaha, kuanzia aina ya watu wanaokuzunguka, mandhari yake, ufikikaji na vitu vingine muhimu. Utulivu huo si tu kwako, bali na kwa familia yako kwa wale wenye nazo.



Watu wengi hasa tunaopanga, huwa tunakosa utulivu tunapotafuta nyumba za kupanga kutokana na kutokujipa muda wa kutosha kutafuta nyumba hizo, hivyo wakati mwingine tunajikuta katika wakati mgumu baada ya kuhamia kwenye nyumba. Hiyo ni baada ya kubaini kwamba ama hazikuendana na sisi au zinaendana nasi lakini mazingira yanayozunguka nyumba si rafiki.

Na kwa sababu hiyo, watu wengine hulazimika au kutamani kuhama kwenye nyumba ndani ya muda mfupi hata kama pesa ya pango waliyolipia haijaisha.

Moja ya vitu vinavyosababisha watu watamani kuhama kwenye nyumba kabla ya wakati ni pamoja na aina ya majirani wanaowazunguka, kwamba baadhi yao ni wakorofi mpaka kufikia hali ya kukosesha amani na utulivu, kwamba kila siku migogoro haiishi, wanaanzisha jipya kila wakati.

Hata mwenye nyumba mwenyewe anaweza kuwa chanzo cha wewe kutamani kuhama nyumba yake kwa sababu ya 'chokochoko' zake za hapa na pale, au ukahamia lakini ukabaini kwamba eneo iliyoko nyumba kunafanyika mambo ambayo ni kinyume cha wewe au na imani yako, kwa hiyo ikakukosesha amani.

Kutokufanikiwa kutimiza ndoto ya kuishi kwenye nyumba zilizo katika mazingira yanayoendana nasi hunasababisha hata ufanisi katika utendaji kazi wakati mwingine kupungua.

Wakati wote mtu anawaza atakumbana na lipi lingine jipya au kutokuwa na uhakika na amani ya familia yake. Kwa hiyo ni muhimu kuishi kwenye nyumba zilizo katika mazingira yanayoendana na sisi.

## kioo kinabadili mwonekano wa nyumba yako

**Na Restuta James**

WATAALAM wa mapambo wanaeleza kuwa ujenzi wa nyumba hauishi, kwamba ni kazi ya kila siku; hili halina ubishi kwani nyumba ni sehemu ambayo mkazi anapaswa kupafurahia na ndio maana kila wakati mwenye nyumba anabadili mwonekano ndani na hata nje.

Katika mwendelezo wa makala za mapambo ya ndani, leo tunakuletea maajabu ya pambo la kioo na nguvu yake katika kubadili mwonekano.

Wataalam wanaeleza kuwa kioo ni pambo ambalo limetumika kwa karne kadhaa na halichuji.

Inaelezwa kuwa kioo kikitumika kupamba chumba kidogo kinabadili mwonekano na kuwa 'kikubwa' na chenye mvuto.

Eneo likiwa kubwa, kioo kinaweza kulibadili na mtu akaliona la kawaida na lenye kuvutia hata kama uhalisia hauko hivyo

Jambo la kwanza la kuzingatia unapotaka kutumia kioo kama pambo ni ukubwa wa chumba na wa kioo pia. Mathalani, usitundike kioo kikubwa sebuleni kuliko sofa ambalo liko kwenye ukuta husika wala kisiwe kidogo kuliko nusu ya sofa hilo.

Katika eneo la sofa, urefu wa kioo sio tatizo sana bali upana na kinatakiwa kuwekwa nchi sita toka linapoishia sofa lako.


Vioo vidogo vina vionjo vyake kama vikiwekwa vingi sehemu moja. Muhimu zaidi ni kupima kile kitakachokuwa kinaonekana kwenye kioo muda mwingi. Wengine hupenda kuweka ua picha itakayoonekana zaidi kwenye kioo.

Jambo lingine unalopaswa kuzingatia ni eneo lenye mwanga. Inaelezwa kwamba kioo kinachotumika kama pambo kikiwekwa karibu na dirisha kinaongeza nuru ndani hivyo kuongeza umaridadi hasa katika chumba kidogo.

Eneo la kona linatajwa kufaa sana kuwekwa pambo la kioo kwani kitaonesha ukuta mwingine na mgeni anaweza kudhani ukuta unaendelea na hivyo kuongeza mvuto. Kona ikiwa inatazama mlango inanoga zaidi.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... 'USO UMEUMBWA NA HAYA LAKINI HAUSAHAU MEKAPU'

# Kiongozi wa RSF aonekana hadharani mara ya kwanza

**KHARTOUM,** SUDAN

KIKOSI cha wanajeshi wa kazi maalum wa Sudan (RSF) kimetoa video ya kiongozi wake Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, akiwahutubia wapiganaji wake.

Hiyo ni mara ya kwanza kwa kiongozi huyo kuonekana tangu mapigano yalipoibuka mwezi Aprili mwaka huu.

Jenerali Dagalo, anayejulikana kama "Hemedti", alionekana kwenye video hiyo iliyochapishwa katika ukurasa wa Twitter, akionekana mwembamba.

Hata hivyo, wachambuzi wanasema mkono wake mmoja ulionekana kama hauko sawa.

Kumekuwa na uvumi kuwa kamanda huyo ambaye ana umri wa miaka 40 hivi amejeruhiwa katika vita hivyo.

Hotuba yake ilijumuisha matamshi yake ya mara kwa mara dhidi ya Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, mkuu wa jeshi ambaye anakabiliana naye katika mzozo wa kupigania utawala wa nchi hiyo. Alisema iwapo uongozi wa jeshi hilo utabadilika, atakubali makubaliano ya amani ndani ya saa 72.

Hemedti aliingia madarakani kwa mara ya kwanza kupitia safu ya wanamgambo wa Janjaweed, wanaotuhumiwa kwa mauaji ya kikabila wakati wa mzozo wa Darfur.

RSF iliundwa na Rais wa zamani Omar al-Bashir, ambaye aliondolewa madarakani kufuatia maandamano ya umma mwaka 2019.

Kiongozi wa RSF aliunga mkono kuondolewa kwake kama njia ya kujiingiza katika nafasi yenye nguvu zaidi.

Lakini muungano wake na Jenerali Burhan ulisambaratika vibaya miezi mitatu iliyopita.

Tangu vita kuanza, wanamgambo wa RSF wamehamia katika maeneo ya makazi ndani ya miji mitatu inayounda mji wa Khartoum, ambao ni Bahri, Khartoum na Omdurman.

Akiwa amezungukwa na wapiganaji wenye silaha katika kanda hiyo ya video ya dakika tano, alikanusha kuwa wale wanaotuhumiwa kwa uporaji mjini Khartoum na kwingine walikuwa wanachama wa RSF.

**BBC**



Kiongozi wa kikosi cha RSF, Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, akionekana kwa mara ya kwanza wakati akizungumza na wapiganaji wake juzi. **PICHA: BBC**

# Watu tisa wajeruhiwa kwa makombora

**KYIV, UKRAINE**

WATU tisa wamejeruhiwa wakiwemo watoto wawili baada ya makombora kushambulia majengo mawili katika mji wa Dnipro mashariki mwa Ukraine.

Waandishi wa BBC walioko nchini humo wamethibitisha kuwa jengo hilo la makazi lilikaribia kuharibiwa kabisa katika shambulio hilo la Ijumaa jioni.

Rais Volodymyr Zelesky, alisema jengo la idara ya usalama ya Ukraine (SBU) pia lilishambuliwa.

Alilaumu kitendo hicho kuwa ni cha kigaidi kutoka kwa Russia.

Kiongozi huyo alichapisha video kwenye mtandao wa Telegram ikionyesha moshi ukipaa juu kutoka kwa majengo yaliyoharibiwa.

Alisema ameitisha mikutano ya dharura na SBU, wizara ya mambo ya ndani, huduma za dharura na maafisa wa eneo kufuatia tukio hilo.

Mkuu wa mkoa Serhiy Lysak alisema kuwa watoto wawili, wenye umri wa miaka 14 na 17, walikuwa miongoni mwa waliojeruhiwa.

Aliongeza kuwa walikuwa wakitibiwa nyumbani.

Hakuna vifo vilivyoripotiwa kufuatia shambulio hilo lililofanyika saa saa mbili usiku kwa saa za Ukraine.

Shambulio hilo la Russia lilikuwa la tatu dhidi ya jengo la SBU, kulingana na Meya wa Dnipro, Borys Filatov.

Alisema majengo yote mawili kwa kiasi kikubwa yalikuwa hayana watu, na jengo la makazi lilikuwa limekamilika hivi karibuni.

**BBC.**

# Trump ajigamba ana uwezo mkubwa kuingia Ikulu 2024

**WASHINGTON,** MAREKANI

WATIA nia kiti cha urais wa chama cha Republican, wameshiriki mkutano wakiwa pamoja kwa mara ya kwanza katika mchakato wa kupata nafasi ya kwenda Ikilu mwakani.

Wagombeaji hao walikutana katika hafla ya kampeni iliyofanyika katika jimbo la Lowa.

Wapinzani wakuu ndani ya chama hicho, Donald Trump na Ron DeSantis waliongoza hafla hiyo ya kila mwaka maarufu kama Lincoln Dinner.

Wagombea wote 13 walipewa dakika 10 za kuzungumza wakati wa hafla hiyo.

Kura za maoni zinaonyesha kuwa Trump anaongoza dhidi ya wapinzani wake licha ya kukabiliwa na changamoto za kisheria.

Aliwaambia waliohudhuria kuwa yeye ndiye mgombea pekee ambaye anaweza kushinda uchaguzi wa mwaka ujao na kudai kuwa hiyo ndiyo sababu pekee ya yeye kukabiliwa na msururu wa mashtaka ya jinai.

Trump amesisitiza kuwa atawania kiti hicho na kwenda Ikulu ya White House, hata kama atapatikana na hatia.

Kulikuwa na zaidi ya watu 1,200 katika katika hafla hiyo, ambayo iliwajumuisha wagombea wote ambao wana ushawishi mkubwa.

**BBC**

# Marekani kumuunga mkono rais aliyepinduliwa Niger

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, ametangaza kumpa msaada wa dhati rais wa Niger aliyeondolewa madarakani Mohamed Bazoum.

Blinken amewatahadharisha wanaomshikilia kiongozi huyo kuwa, msaada wa kifedha wa mamilioni ya dola kwa taifa hilo uko hatarini.

Taarifa ya msemaji wa wizara hiyo, Matt Miller ilisema Blinken ametangaza kwa mara nyingine kuwa Marekani inamuunga mkono Bazoum.

Alisema hayo wakati Blinken alipokuwa akikamilisha ziara yake katika mataifa kadhaa ya ukanda wa Pasifiki juzi Ijumaa.

Matamshi ya Blinken yametolewa siku moja baada ya Jenerali Abdourahamane Tchiani kujitangaza kuwa kiongozi mpya wa mpito wa Niger baada ya mapinduzi ya kijeshi yaliyotokea Jumatano wiki hii.

**DW**

# Kiongozi wa upinzani Senegal akamatwa na maafisa usalama

KIONGOZI wa upinzani nchini Senegal, Ousmane Sonko amekamatwa baada ya kuvutana na maofisa wa usalama waliokuwa wamezingira makazi yake.

Mwanasiasa huyo alikamatwa jana baada ya kutokea mvutano na askari hao waliokuwa wamezingira nyumba yake kwa siku nzima.

Awali Sonko mwenye (49), aliandika kupitia mtandao wa X, zamani ukijulikana kama Twitter, kwamba wanajeshi walimchukua video kwa kutumia simu zao wakati alipokuwa akirejea kutoka Msikitini na kusababisha purukushani baina yake na maafisa wa usalama aliowataka kufuta video zake.

Sonko alihukumiwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili jela mnamo mwezi Juni, hukumu ambayo ilisababisha maandamano yaliyoambatana na vurugu.

Hukumu hiyo ilitia doa nia yake ya kuwania urais katika uchaguzi wa mwaka ujao.

Mwanasiasa huyo alisusia kesi mahakamani na kusalia nyumbani kwake mjini Dakar tangu hukumu hiyo itolewe, akidai vikosi vya usalama vilivyokuwa nje ya nyumba yake vinamzuia kuondoka.

## MAKALA

# KUKUBALI MAKOSA NA KUSAHIHISHA SI UDHAIFU



Na Magabilo Masambu

**Kusema hivyo haikuwa udhaifu lakini ulikuwa uimara kwa sababu pengine angeficha na akachaguliwa kuwa Rais wa nchi, inawezekana ingetokea siku moja mtu akasema huyu Rais amewahi kuvuta bangi.**

KATIKA kitabu cha TUJISAHIHISHE, kilichoandikwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1962, kina maneno yanayosema: "Watu walio katika hatari kubwa ni wale ambao wanafikiri kuwa wanajua kila kitu na hawana haja ya kujifunza zaidi. hii ni tabia mbaya ambayo huzuia kabisa maendeleo"

Kutokana na maneno hayo, ni wazi kwamba hakuna anayejua kila kitu na kama ndivyo, basi hakuna mkamilifu, hivyo tunakosea kila siku katika kuwaza na kutenda kwenye shughuli zetu za kila siku.

Kumekuwapo na kasumba au tabia iliyojengwa katika mila na desturi zetu kwamba mkubwa hakosei au kiongozi hakosei hasa katika jamaii yetu ya kiafrika na ikitokea mtu au kiongozi fulani akafanya makosa na kisha akaomba msamaha, inaonekana kwamba ni dhaifu.

Ukweli ni kwamba kiongozi akifanya makosa na akayaona makosa hayo, akafikia hatua ya kuomba radhi juu ya makosa yake, huo utakuwa si udhaifu bali ni ukomavu wa fikra.

Faida kubwa ya kuyaona makosa na kuomba radhi huwa ni mwanzo wa kujifunza mambo mapya na kuonyesha uungwana na utu wako kama kiongozi. Katika kitabu cha TUJISAHIHISHE, Nyerere ameyataja makosa mengi ambayo mara nyingi yanafanywa na viongozi au na wale wanaokuwa na dhamana ya kimamlaka mahali popote.

Yeye mwenyewe binafsi anakiri kwamba kuyataja makosa hayo lakini haimaanishi kwamba yeye hakuwa na makosa hayo. Anasema waziwazi kuwa ama amewahi kuyafanya au aliendelea kuyafanya na anasema: "Katika kosa kubwa tunalofanya ni kutaja makosa tusiyo nayo na kuficha makosa tuliyo nayo sisi wenyewe."

Kukiri kutolifahamu jambo ni mwanzo mzuri wa kujifunza. Tukishatambua kwamba hatujui basi ulazima wa kusikiliza ushauri na kukoselewa unakuwapo. Viongozi wazuri huwa wanakubali udhaifu wao na kwa kufanya hivyo ni mwanzo wa mabadiliko kuelekea maendeleo katika mwelekeo chanya.

Rais mstaafu wa Marekani, Barack Obama, wakati wa kampeni za urais, alikiri kwamba katika ujana wake aliwahi kuvuta bangi. Kusema hivyo haikuwa udhaifu lakini ulikuwa uimara kwa sababu pengine angeficha na akachaguliwa kuwa Rais wa nchi, inawezekana ingetokea siku moja mtu akasema huyu Rais amewahi kuvuta bangi.

Yapo makosa ambayo tunayafanya tukiwa na wengine, hivyo hayawezi kuwa siri tena na ikiwa kiongozi utayafanya kuwa siri basi hilo litakuwa anguko lako. Simaanishi kwamba kila ulilonalo uliseme. Yapo mambo ambayo unayasema kwa faida yako mwenyewe ama kwa faida ya umma au kwa masilahi mapana ya nchi.

Kiongozi yeyote anapochaguliwa au kuteuliwa kuwa mtumishi wa mahali fulani, haimaanishi amepimwa na kuonekana anajua sana kufikiri kuliko wengine bali sababu za uchaguzi au uteuzi wake zinaweza kuwa nyingi kama vile urafiki, mapenzi, rushwa, kujikomba, uwezo binafsi na elimu. Haimaanishi kwamba akishachaguliwa au kuteuliwa basi hatendi makosa na kwamba hata kama anatenda makosa hana sababu ya kukubali.

Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha TUJISAHIHISHE, anasema tena: "Demokrasia haiwezi kudumu ikiwa wachache hawatakubali matakwa ya wengi, lakini matakwa ya wengi hujulikana katika majadiliano au mazungumzo ya waziwazi, kadhalika matakwa ya wachache hujulikana katika majadiliano na mazungumzo bila wale wachache kusema waziwazi matakwa yao majadiliano hayana maana."

Kwa msingi huo, ni kwamba katika majadiliano au mazungumzo ndipo mahali aliyetenda makosa anapokiri makosa yake wala hautakuwa udhaifu.

Kuna wakati tunajaribu kupima ukweli wa jambo kwa kutazama wingi wa watu wanaolitetea, lakini ni muhimu kupima ukweli na uhalisia wa jambo lenyewe.

Kuna wakati pia tunashindwa kuwatetea wadogo wanaoonewa japo tunajua wazi hawana makosa na kuwasifu wakubwa ilhali tunajua wanakosea. Uimara wa hoja juu ya ukweli wa jambo vilevile haujengwi kwa wingi wa maneno bali ukweli.

Ikiwa wapo watu wanapiga kelele dhidi yako ukiwa kiongozi mahali fulani, lazima utafakari juu ya yale wanayopigia kelele na hayawezi kudharauliwa kwa sababu wanaopiga kelele ni wachache.

Uchache wao lazima upimwe kwenye mambo yenyewe, si wingi wao bali hoja zao.

Ukiona zina msingi basi huna budi kukiri kwamba katika eneo linalopigiwa kelele umefanya makosa, hivyo unahitaji kujisahihisha ili wanaopiga kelele wasiwe wengi maana ukisubiri kelele zizidi basi inaweza kuleta wakati mwingine tafrani ambazo zingeweza kuzuiwa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Penye penzi hapakosi tezi, bila ya vizabizabina hamna mapenzi*



Na Adam Fungamwango

WASWAHILI wanasema bila usiku hakuna mchana, bila mwezi hakuna jua na binadamu wote waliofanikiwa ni lazima walipitia kwenye changamoto.

Ili binadamu afanikiwe, abadilike au ajue kitu alichonacho ni cha thamani ni lazima apitie misukosuko fulani ambayo itamfanya ashtuke na kubadilisha mtazamo na msimamo wake.

Kwenye mapenzi au ndoa nako ni hivyo hivyo kupitia changamoto ni lazima ili wahusika wakomae na waweze kujirekebisha na kujiboresha.

Ukiona penzi lolote linakwenda tu bila watu kutia fitina, uchonganishi, wivu, zengwe, au maneno maneno, basi inabidi mjitafakari upya.

Hilo itakuwa ndoa au penzi la kawaida sana ambalo haliwashughulishi watu kwa namna yoyote ile, badala yake wanataka liendelee ili waone vituko au kile ambacho wanapenda kukiona kutoka kwa wapenzi hao.

Na mara nyingi itakuwa kitu kibaya, sababu mara nyingi binadamu hawapendi kuona watu wanaishi vizuri kwenye mapenzi au ndoa zao.

Ndiyo maana narudia tena, ukiona ndoa au penzi lipo tu, hakuna mtu anayelitilia fitina, uongo, chuki au kutaka kuwatenganisha hapo hakuna kitu. Itabidi tu mjitazame upya.

Ndoa imara au penzi la kweli ni lazima tu liwe na baadhi ya watu ambao kwa sababu zao binafsi watalifuatilia, watalipiga vita na kulifanyia kila aina ya vitimbi ili lisambaratike kwa sababu linawakera.

Ukiona ndoa au penzi lako linapigwa sana vita ujue ni la ukweli, madhubuti, hivyo linawaumiza watu na wanachotaka ni kuliharibu, kulivunja ili kuondoa kile kitu kinachokupa furaha.

Mara nyingi maneno yanaanza kupenyezwa huku na huku. Mmoja ataambiwa hili na mwingine lile.

Msipokaa imara au kutambua kuwa maneno maneno au fitina huwa yapo kwenye ndoa au mapenzi, ni rahisi sana kutengana.

Vijana Jazz Band miaka ya 1990, walifyatua kibao cha kimoja wakakiita 'Sabetina', utunzi wake Athumani Momba (marehemu) aliimba.

"Ndoa ina tamu na chungu unielewe hivyo mpenzi wangu ee, tunapooana tutafanya sherehe kubwa lakini kumbuka maisha ya ndoa yana tamu na chungu, tusiyafuate maneno ya wambea, tusiyafuate maneno ya pembeni, yataharibu bure, ndoa yako.

Uvumilivu kwenye ndoa ni muhimu Sabetina, hakuna ndoa inayokosa misukosuko, Sabetina.

Uvumilivu ni alama ya ushujaa Sabe katika ndoa yako eee, kwani ngome ya mapenzi, haivunjwi na fitina, Sebatina."

Ni mashairi murua yaliyomo kwenye kibao hicho. Yoyote anayeingia kwenye ndoa au mapenzi kama hawezi kuhimili misukosuko ya wambea na vinenoneno vya uongo na kuamini kila anachosikia, basi hawezi kudumu kwenye mahusiano kwa muda mrefu.

Atakuwa mtu wa kuhangaika na kujiona kama ana mkosi.

Cha muhimu ni kuwaona vizabizabina ni kama mbu wanaopiga kelele nje ya chandarua.

Narudia kwa kusema yoyote anayeingia kwenye mahusiano, iwe ndoa au mapenzi atarajie kukutana na watu hao ambao ndiyo mkate na siagi kwenye mapenzi. Ukiona penzi linakwenda tu kama gari lipo kwenye barabara ya lami, muanze kujichunguza wenyewe, kuna kitu hakijakaa sawa hapo.

Vizabizabina na vilata wa mtaa ndiyo chachu yenyewe kwenye ndoa na mapenzi na kama wakitokea wapenzi wawili wakawa wote wanalifahamu hilo basi watakuwa wanainjoi sana kwa sababu kashikashi zao ndiyo zitakuwa zinawaweka pamoja na kuzidi kuwakera, ili wakereke zaidi.

Watatoka kila wiki endi, watavaa nguo nzuri, watakula chakula kizuri, ili kuendelea kuwakera, hilo linafanya pia penzi kuzidi kunoga na kukomaa zaidi

Ndiyo maana Juwata Jazz Band wakaimba siku zote penye penzi hapakosi tezi, na huwezi kula muwa bila kukuta fundo.

Wimbo huu ulitingwa na marehemu Suleiman Mbwembwe mwaka 1989 akiwa na Msondo Ngoma.

"Penzi letu halikuanza zamani naye Mwajabu, na wala kamwe hatufanyi vishindo ooh mama, lakini watu wamenza maneno yao, ndiyo maana mwanzo nilisema mlisikia, kwa kuwa tunapendana mengi utasikia lakini usijali eee. Kwa kuwa tunapendana mengi utasikia, lakini usijali ee."

Hiyo ni beti ambayo mwanaume anaelezea kuwa alitambua mapema kuwa wambea watalitikisa penzi lao, hivyo akamtahadharisha bibie. Mwanamama naye akamjibu mpenzi wake kwa beti hii.

"Mimi sina wasiwasi bwana, naelewa, nimeyazoea, nimeshakuwa mtu mzima, naelewa penye penzi hapakosi tezi, wakale walisema na huwezi kula muwa, bila kukuta fundo.

Hata leo naeleza mbele yao wasikie hehe. Wasikie mama maneno maneno mama eee.

Naelewa kuwa bwana huyu bado kijana. Mama mama mama mama ee, kuna wapenzi wengi kabla yangu ambao wanakupenda, hata hivyo moyo wangu wampenda.

Na hizi ni dalili kwamba, roho zenu siyo njema kwake. Hata akila vizuri mnasema, anaiba mali ya umma.

Akibadili mavazi mnasema, kijana na anaringa nini? Japokuwa hana ubaya nanyi Mola atamlipia."

Safi kabisa, mwanamke ameshajua lengo la watu ni kumfitinisha jamaa, na akajua lengo kuwa kuna baadhi ya wasichana walikuwa wanampenda kabla yeye hajachukuliwa, hivyo ni fitina tu ili amuache, kijana wa watu abaki anahangaika.

Amewashtukia kuwa bwana yake kila anachokifanya wao wanaona anaringa, yeye hatomuacha na kwa sababu hana ubaya na wafitini, Mola atamlipia tu. Kwa penzi hili, vizabizabina wajifungie ndani tu.

**Tuma maoni 0716 350534**

# HADITHI

# Kafie kwenu-4

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

KAMA kawaida yake, ni mtu mwnye kujiamini na kujaribu licha ya uonekano wake duni.

"Habari yako bibie!" Akasalimia, akiwa tayari kujibiwa lolote lile.

Salamu haikujibiwa haraka. Carry aliyekuwa amevaa blauzi ya nyeupe yenye madoa meusi iliyomkaa vema na sketi ya bluu fupi iliyoacha sehemu ya mapaja yake wazi alimtazama kama mtu ambaye anajaribu kumkumbuka amemuona wapi.

Hata hivyo, bado uangaliaji wenyewe ulikuwa wa dharau.

"Umenisahau dada? Mimi si yule ambaye majuzi tulikutaka kule Kinondoni Moscow chini kidogo hivi? Tena siku hiyo ulikuwa na dada yako." Ilionekana kama Carry kamkumbuka hivi.

"Hivi kwa nini wewe kama unapenda kutufuatilia, kuna kitu unatudai?"

"Hapana dada."

"Sasa mbona unapenda kutufuatilia mimi na dada yangu, haya siku ile sijui mwenyewe unasema umetusalimia, leo nini tena kimekutuma unisalimie?"

"Dada kwani salamu inagombwa?"

"Wee, koma, aliyekwambia anataka kusalimiwa nani? Kama kusalimiwa mali si ningekuwa nimejaza mapesa ndani."

"Mimi sifanyi hivi kwa ubaya, ina nataka tu kuwasalimia tufahamiane."

"Enhee, unataka kunifahamu vipi?" Carry alionekana kutulia ili kumpa nafasi ya kufahamiana. Lakini kwa jinsi alivyokuwa anamwangalia huku akiwa amemshikia kiuno mikono yote miwili ilimuwia vigumu mno James kuongea. Kwa sababu alijua kwa jinsi ilivyo hata akiongea nini sidhani kama atakubaliwa.


"Najua nakuchelewesha." Akaanza kuongea kwa namna ya woga na kigugumizi.

"Ongea vizuri wewe, ningekuwa nachelewa nisingesimama hapa."

"Unajua dada wewe ni mzuri sana, mrembo sana sijaona mwanamke aliyejaaliwa uzuri, aliyeumbwa akaumbika kama wewe katika eneo lote hili kuanzia Kinondoni Mkwajuni hadi Moscow."

"Kwa hiyo, ndiyo unataka kusemaje?" Akauliza kwa dharau akigeuza uso wake kwanza akaangalia sehemu nyingine, halafu akaurudisha kumtazama mzungumzaji kwa namna ya nyodo.

Niseme tu nimetokea kukupenda Carry." "We, koma, ishia hapo hapo, kwanza nani kakutajia jina langu?"




"Wewe unajulikana huku kila mtu anakufahamu, kwa nini nisilijue?"

"Kwanza nimekuheshimu wewe kikaragosi, huna hadhi ya kuongea na mimi."

"Inawezekana, lakini naomba unipe hiyo nafasi tafadhali." Bado sauti yake ilikuwa ya mtu asiyejiamini kutokana na kupata upinzani mkali na dharau kutoka kwa Carry.

"Mimi ni mstaarabu na mwema sana, hutojutia kuwa na mimi, nikubalie." Aliendelea kuomba akiwa hamuangalii Carry usoni.

Ghafla kikafuatia kicheko cha kejeli na dharau kutoka kwa Carry. Halafu akamuuliza kwa sauti, "unasema?"

Ile sura ya ukali na hasira usoni mwake ilitoweka na kubakia ya tabasamu ambalo pamoja na kwamba halikuwa halisi, lakini lilimfanya kuvutia na kuzidi kuonekana mrembo.

"Naomba uwe mpenzi wangu." Akajibu James.

"Naomba uwe mpenzi wangu." Carry akarudia neno hilo kwa namna ya kejeli huku akiwa amebana pua moja kwa kidole.

Wakati huo uso wake aliugeuza na kuangalia sehemu nyingine, alipomaliza kumuiga, akamshikia tena kiuno na kumtazama usoni.

"Hivi kama nikikukubalia kikaragosi wewe, utanipa nini? Hivi unavyojiona." Akanyamaza lakini kidole chake akawa anakionyesha kwa James akikishusha na kukipandisha kiasi cha mara nne hivi.

"Umeniona mimi nilivyo? Hivi unaweza kunihudumia ikiwa wewe mwenyewe tu huwezi kujihudumia hapo ulipo."

"Carry, duniani watu hawafanani..."

"He he he, we bwana koma kuniitaita jina langu, unataka kila mtu alijue, nimekustahi kwa pua tu hapa nimesimama napoteza muda juu yako, halafu unataka kunichefua tena, samahani eee."

"Basi samahani dada." James bado alikuwa kwenye wakati mgumu akibananishwa kwenye kona na msichana mrembo, Carry.

"Enhee, ulikuwa unasemaje vile, maana hata nimeshasahau tulikuwa tunazungumza nini."

"Si nimekwambia mimi nakuhitaji?" Akajitutumua.

"Kaka ukome ee." Haikwenda hivyo hivyo, akamalizia kwa kumtia singi.

James alibaki mpole kama kawaida yake hakutaka kufanya kitu chochote. Jambo alilichokoza mwenyewe. Amelikoroga ni lazima alinywe.

Uso wake ulikuwa amejikunja na kusawijika kwa maneno ya kila aina ya dharau, ufedhuli, unyanyasaji na ukosefu wa adabu.

"Hivi wewe vitu hivi vya thamani nilivyovyaa unaweza kuninunulia wewe?"

James akajitutumua tena na kujibu. "Nitajitahidi tu, nitapambana kadri ya uwezo wangu ili kuweze kutimiza mahitaji yako."

**"Hivi wewe vitu hivi vya thamani nilivyovyaa unaweza kuninunulia wewe?" James akajitutumua tena na kujibu. "Nitajitahidi tu, nitapambana kadri ya uwezo wangu ili kuweze kutimiza mahitaji yako."**

Carry akamtazama James kwa namna ya dharau na huruma ya mzaha, halafu akaangua kicheko.

"Yaani unanichekesha wewe! Hivi unajua unachokiongea wewe?" James hakujibu kitu.

"Siwezi kutembea na wewe unasikia?" Sasa aliongea na sauti ya chini, lakini nzito na yenye msisitizo.

"Huna hadhi ya kuwa mpenzi wangu sawa?" Akamuonyeshea kidole cha shahada.

"Mimi naenda zangu, sitaki kurudiarudia kuongea, sasa nasema ukome kunifuatafuata au kunisimamisha au hata kuniita jina langu. Ukinioна tupishane kama hatujuani, uniheshimu kama chongo la mkweo."

"Sawa nitafanya yote hayo unayosema, samahani sana, lakini mimi nakupenda na nitaendelea kukupenda."

"Hivi wewe baba una wazimu?" Akawa kama amepandishwa tena mashetani kwani alirudia kuongea kwa sauti kubwa na ya hasira tofauti na ile ya dakika chache za mwisho.

"Unampenda nani we masikini? Hivi wewe, au hunioni vizuri, una tatizo la macho? Hebu niangalie kwanza. Unaniona nilivyo." Carry akaanza kuanza kugeuka kwa madaha akimuonyesha uzuri aliojaaliwa na mwenyezi Mungu.

"Umeniona eee, haya, umeridhika? Kama umeniona vizuri nadhani akili yako lazima ikuambie kuwa hii siyo taipu yako. Kwamba mbaya, hauvutii..."

"Basi! Usiendelee tena, maana unaendelea kunidhalilisha barabarani, afadhali tungekuwa ndani dada." James alionekana kama kuchoshwa na ukali wa maneno ya Carry.

Maneno hayo yalionekana kumkasirisha Carry. Akacheka kicheko ambacho si halisi. Ni cha hasira.

"Sasa hapa aliyemdhalilisha mwenzake nani? Wewe ndiyo umenidhalilisha kwa kusimama hapa na kikaragosi kama wewe. Narudia tena ukome, usinichoshe, usinichoshe, tusichoshane, kwa heri ya kuonana, hebu nipishe mie." Akaondoka Carry kwa hasira na kumsukuma kwa kutumia mwili James.

Pamoja na kwamba mwili wake ulikuwa mwembamba na laini lakini alifanikiwa kumtingisha James akapepesuka nusu kuanguka.

Mwili wake pamoja na kwamba ni mkakamavu ulikuwa umeshanyong'onyea kwa maneno aliyovurumishiwa na Carry.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# JACQUELINE WOLPER

## WATOTO WAMEMBADILISHA

MWIGIZAJI mkongwe katika bongo muvi, Jacqueline Wolper, amesema watoto wamembadilisha tabia na kuwa mwanamke mwenye mapenzi mazito.

Amesema, kuwa na mtoto ni jambo lingine, kama huna upendo na mapenzi huwezi kuwa na malezi bora na yanayofuata maadili.

"Watoto wangu nawapenda sana, ratiba zangu wamezibadilisha. Tangu 2019 nilianza kubadilika wakati nilihitaji kuwa mama, nilivyopata watoto nimebadilika sana," amesema.

## *Hakuna kama Burna Boy*

MWANAMUZIKI nyota kutoka Nigeria, Burna Boy anazidi kuonyesha yeye ndiye mwamba baada ya kutoa wimbo mkali Big 7, ambao sasa umewashika mashabiki.

Kuachiwa kwa wimbo huo, ni hatua ya mwisho ya kukamilisha albamu yake mpya inayoitwa 'I Told Them' ambayo itatoka Agosti 24.

"Big 7, imetayarishwa na kampuni ya MDS ambayo ni maarufu kwa kutoa nyimbo zinazovutia.

Video ya muziki kibao hicho imeongozwa na mtengenezaji wa filamu maarufu Benny Boom.

## ZISIKUPITE

### RAYA ATAKIWA UJERUMANI
KLABU ya Bayern Munich imeanza mazungumzo na Brentford kuhusu mpango wa kumnunua kipa wao, David Raya mwenye umri wa miaka 27, huku mlinda mlango wa Uswisi, Yann Sommer mwenye miaka 34, akijadili kuhamia Inter Milan. (***Sky Sports***)

### MANE ANUKIA AL NASSR
BAYERN Munich pia imekubali ombi la Al-Nassr kumnunua mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 31. (***Fabrizio Romano***)

### KANE NA BAYERN
MAAFISA wa Bayern hawatasafiri kwenda London kukutana na wawakilishi wa Tottenham kuhusu mpango wa kumnunua mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri was miaka 30, lakini klabu hiyo ya Ujerumani bado inawasiliana na Spurs. (***Sky Sports***)

### SPURS YAMTAKA TEL
TOTTENHAM Hotspur itatumia mazungumzo yao na Bayern kuhusu Harry Kane kujadili nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa klabu hiyo ya Ujerumani mwenye umri wa miaka, 18 Mathys Tel. (***Telegraph***)

### LUKAKU KUUZWA KABISA
CHELSEA imekataa ombi la Juventus la kutaka kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30 kwa sababu wanataka kumuuza kabisa. (***Tuttosport***)

### DEMBELE HUYO PSG
KLABU ya Paris St-Germain inakaribia kukamilisha dili la kushtukiza kumsajili winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele kutoka Barcelona. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 ana kifungu cha kutolewa cha euro milioni 42.8 ambacho kinamalizika Jumatatu. (ESPN)

### CHELSEA WAKATAA
CHELSEA wamekataa ombi la Juventus la kutaka kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku. (***Mail***)

### MAXIMIN AUZWA
KLABU ya Newcastle United imemuuza winga Mfaransa, Allan Saint-Maximin mwenye umri wa miaka 26 kwa Al-Ahli ya Saudi Aarabia kwa euro milioni 30. (***Mail***)

### HENDERSON KWENDA FOREST
MANCHESTER United wapo tayari kumruhusu mlinda mlango wa England, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 26 ajiunge na Nottingham Forest kwa mkopo. (***Manchester Evening News***)

### PEDRO HASAJILIWI
KLABU ya Aston Villa haitamsajili winga wa Sporting Lisbon na Ureno, Pedro Goncalves mwenye umri wa miaka 25, kwa sababu ofa yao ya juu ya pauni milioni 38.6 ilikuwa pungufu ya bei ya Sporting. (***Recorg***)

### FRED AVUTIWA
KLABU ya Galatasaray inavutiwa na kiungo wa kati wa Manchester United na Brazil Fred mwenye umri wa miaka 30, lakini kuna pengo katika uthamini kati ya klabu hizo mbili. (***Sky Sports***)

### FOREST IMEKATAA
KLABU ya Nottingham Forest imekataa ombi la rekodi ya klabu la pauni milioni 35 kutoka kwa Brentford kwa ajili ya mshambuliaji wao wa Wales, Brennan Johnson mwenye umri wa miaka 22. (***Telegraph***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAN UTD YAKATAA OFA YA KUMUUZA MAGUIRE

**MANCHESTER,** England

●●● Iko tayari kumruhusu beki huyo kuondoka ikiwa kutakuwa na timu itakayotoa ofa nzuri inayofikia....

MANCHESTER United imekataa dau la pauni milioni 20 kutoka West Ham kwa ajili ya Harry Maguire, vyanzo vimeiambia ESPN.

Man United ipo tayari kusikiliza ofa, lakini watamruhusu tu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kuondoka ikiwa ofa muhimu itatolewa.

**Beki huyo wa England ana thamani ya karibu pauni milioni 40 na ikiwa haitafikiwa kocha, Erik ten Hag ana furaha kum bakisha mchezaji huyo wa zamani wa Leicester kwa msimu ujao.**

Ten Hag amekuwa akiwatumia zaidi Lisandro Martínez na Raphaël Varane kama mabeki wa kati na Mholanzi huyo alimvua unahodha Maguire mapema msimu huu wa joto, lakini anataka angalau mabeki wanne wa kati kwenye kikosi chake.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba West Ham wanazingatia hatua yao inayofuata lakini wanasita kutoa ofa zaidi ya kile ambacho tayari wametoa.

Hata kama ofa ya West Ham itakubaliwa, jambo lingine la kushikilia ni mshahara wa Maguire.

Ana miaka miwili pamoja na chaguo la mwaka mmoja kwenye mkataba wake na mshahara wake utaongezeka msimu huu wa joto baada ya United kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United haitazamii kumwachia Maguire lakini atapata chaguo la kuhama ikiwa ofa kubwa itatolewa. Hali hiyo hiyo inatumika kwa Scott McTominay, ambaye pia anasakwa na West Ham.

Wakati huohuo, United wametoa ofa ya takribani pauni milioni 51 kumnunua mshambuliaji wa Atalanta, Rasmus Höjlund.

# Mahrez mali ya Al Ahli

**RIYADH,** Saudi Arabia

RIYAD Mahrez amekuwa nyota wa hivi karibuni zaidi kuhamia Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, baada ya kukamilisha uhamisho wa kwenda Al Ahli kutoka Manchester City.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England walikubali mkataba wa pauni milioni 30 na Al Ahli kwa Mahrez, ambaye alikuwa na nia ya kucheza nchini Saudi Arabia.

Mkataba huo unajumuisha malipo ya uhakika ya pauni milioni 26 pamoja na nyongeza nyingine ya pauni milioni 4.

Mahrez alishinda mataji manne ya Ligi Kuu England akiwa na City, yakiwemo mataji matatu msimu uliopita.

Alicheza mechi 236 tangu ajiunge nayo kutoka Leicester City mwaka 2018.

"Kuichezea Manchester City imekuwa heshima na fursa nzuri," alisema Mahrez akiiambia tovuti ya City.

"Nilikuja City kushinda mataji na kufurahia soka langu na nilifanikisha hayo yote na mengine mengi.

"Nimekuwa na miaka mitano isiyoweza kusahaulika na klabu hii ya soka, nikifanya kazi na wachezaji wa ajabu.

"Nimeweka kumbukumbu nzuri maishani mwangu na namna tulivyoshinda taji la Ligi Kuu ya England na vita ambavyo tumekuwa navyo na Liverpool na, mwaka jana, Arsenal, ilisisitiza hamu na mawazo yetu ya kuwa bora zaidi.

"Manchester City daima itakuwa sehemu kubwa na yenye furaha maishani mwangu."







# DEMBELE AKARIBIA KUTUA PSG

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain iko tayari kukamilisha dili la kushangaza la kumsajili Ousmane Dembele kutoka Barcelona, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mabingwa hao wa Ufaransa wamekuwa wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa muda mrefu, na, kulingana na vyanzo, fowadi huyo tayari amekubali mkataba wa miaka mitano PSG.

Dembele ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 50 katika mkataba wake na Barca ambayo itatumika hadi Julai 31, wakati itapanda hadi euro milioni 100.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa pia ana ofa ya nyongeza kutoka kwa Barca mezani, lakini PSG wana uhakika kwamba mchezaji huyo anavutiwa zaidi na mradi wao.

Kulingana na vyanzo, bado kuna maelezo ya kutatuliwa lakini mazungumzo kati ya wakala wa mchezaji, Moussa Sissoko, na Luis Campos, Mkurugenzi wa michezo wa PSG, ni mazuri.

Vyanzo vya habari viliongeza kuwa kocha wa Barca, Xavi anataka kumbakisha Dembele kwa kuwa anamchukulia kama mchezaji muhimu, lakini anaelewa klabu hiyo inajua kwamba kupokea ada kubwa ya uhamisho kutawasaidia katika masuala yao ya kifedha.

Klabu hiyo ya Katalunya haitaweza kufanya lolote ikiwa Dembélé atakubali kuhama na PSG kulipa kifungu cha kutolewa.

Dembele alisajiliwa kwa wababe hao wa LaLiga kutoka Borussia Dortmund mwaka 2017 kwa dili la thamani ya euro milioni 105, lakini amekuwa akikabiliwa na matatizo ya majeraha wakati alipokuwa Camp Nou.

Fowadi huyo amefunga mabao 40 katika mechi 185 alizochezea Barcelona na ameshinda mataji matatu ya LaLiga nchini Hispania.

Dembélé anakaribia kuwa ujio wa hivi karibuni zadi PSG, ambao wamewasajili Marco Asensio, Manuel Ugarte, Lucas Hernández, Cher Ndour, Lee Kang-in na kocha mpya, Luis Enrique.

# Juventus yafungiwa mashindano ya Uefa

**TURIN,** Italia

JUVENTUS imeondolewa rasmi kwenye michuano ya Ulaya na kuamriwa kulipa faini ya euro milioni 10 kutokana na makosa ya kifedha.

Faini hiyo inaweza kupanda hadi euro milioni 20 ikiwa watashindwa na mahitaji ya haki sawa ya kifedha katika miaka mitatu ijayo.

Nafasi yao katika raundi za awali za Ligi ya Europa Conference itachukuliwa na Fiorentina iliyo nafasi ya nane.

Juventus ilikiuka na mfumo wa udhibiti wa fedha wa Uefa na makubaliano ya suluhu yaliyotiwa saini Agosti 2022.

Klabu hiyo ilipokonywa pointi 10 kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Mei kwa kupandisha ada za uhamisho kwa njia isiyo halali ili kuongeza mtaji.

Hiyo iliwafanya hatimaye kushuka kutoka nafasi ya tatu hadi ya saba, na kufuzu michuano ya Europa Conference.

Kwa kuzingatia hali hiyo, mawakili wa Juve walifanya kazi na Uefa kukubali makubaliano ya rufaa, bila kuwajumuisha kutoka kwenye mashindano ya Ulaya kwa mwaka mmoja.

HABARI MICHEZO

# KAGERA SUGAR KUFUATA MAKALI UGANDA JUMANNE

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar inatarajiwa kuondoka nchini jumanne kwenda Uganda kwa ajili ya kucheza michezo ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya wa ligi kuu inayotarajiwa kuanza Agosti 15.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Ally Masoud amesema safari hiyo ina lengo ya kwenda kusaka makali kabla ya kuanza msimu mpya.

"Tutasafiri na wachezaji na benchi la ufundi lote,tukiwa huko Uganda tutafanya mazoei kwa siku kadhaa na tutacheza mechi tatu za kirafiki," alisema Masoud.

Hata hivyo hakutaja majina ya timu ambazo watacheza nazo, akisema watazitangaza baada ya kufika nchini humo.

Kuhusu maandalizi yanayoendelea hivi sasa alisema kikosi kimeondoka juzi mkoani Kagera kwenda Mwanza ambako watacheza mchezo mmoja wa kirafiki kabla yakuanza safari ya Uganda

"Kikosi kimeshaanza safari taratibu, kimekwenda Mwanza kwa ajili ya mechi za kirafiki na timu za Ligi Kuu siku ya Jumapili (leo) na kama itawezekana Jumatatu pia tutakuwa na mechi na Jumanne tutaondoka," alisema.

Akizungumzia usajili alisema tayari wameshakamilisha idadi ya wachezaji 12 wapya mabao walihitaji kuwasajili kwa msimu huu, huku wakiwa wameacha wachezaji saba.

"Sisi tulishaanza kambi muda tu, tumeshasajili wachezaji 12 wapya na kuwaacha saba," alisema.

Alisema suala la usajili walishamaliza na sasa ni wanafanya maandalizi makubwa kwa sababu hawataki kufanya vibaya kwenye ligi.




Wasanii wa muziki wa kizazi kipya wakitoa burudani katika shindano la miss Tanzania lilofanyika hivi karibuni jijini Dare s Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Ni vita ya ndugu CECAFA leo*

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania Bara ya Wasichana wenye umri chini ya miaka 18 (U-18) inashuka dimbani leo kuvaana na ndugu zao kutoka Visiwani Zanzibar katika mashindano ya kuwania ubingwa kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Mchezo huo unatarajiwa kuchezwa majira ya saa 12:00 ya jioni, baada ya kukamilika kwa mchezo wa kwanza kati ya Ethiopia dhidi ya Burundi utakaopigwa saa 9:00 alasiri, ambapo michezo yote itachezwa kwenye uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam huku Tanzania ni wenyeji wa mashindano hayo.

Tanzania Bara inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi katika michezo yake miwili ilyotangulia ambapo ilianza kwa kuifunga Burundi mabao 2-0 na kushindi mabao 3-0 dhidi ya Ethiopia.

Zanzbibar ambao mchezo wa leo utakuwa wa pili kwao katika michuano ya mwaka huu, itaingia uwanjani ikiwa imetoka kupoteza mbele ya Uganda kwa kukubalikipigo cha mabao 3-0.

Katika mchezo wa leo timu zote zinahitaji matokeo kujiweka sehemu salama ya kuendelea na mashindano hayo huku Tanzania Bara ikidhamilia kutwaa ubingwa wa nichuano hiyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti makocha wa timu hizo kila mmoja amejinasibu kubuka na ushindi.

Kocha wa Tanzania Bara, Bakari Shime alisema ingawa kwao ni mechi ngumu lakini ni lazima wapambane kupata ushindi ili kujiweka katika mazingira mazuri yakufukuzia ubingwa huo.

Alisema licha ya Zanzibar kupoteza mechi ya kwanza hawatawadharau kwa kuwa anaamini mechi ya leo watakuja kivingine kwa kuhitaji matokeo mazuri.

"Hii mechi sio rahisi, tunahitaji kupambana kushinda ninaimani watakuja kivingine tofauti na walivyocheza mechi yao ya kwanza, kikubwa wachezaji wako tayari kwa ajili ya kupambana kusaka ushindi katika mechi yetu ya kesho (leo)," alisema Shime.

Kwa upande wake Kocha wa Zanzibar, Abdulmutik Haji alisema ameshafanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye mechi ya kwanza dhidi ya Uganda na wako tayari kupambania ushindi kwenye mchezo wa leo.

"Tumejiandaa vizuri, wachezaji wangu wako tayari kwa mchezo huu, utakuwa mchezo mgumu na wenye ushindani, lakini hakuna namna lazima tupambane kupata ushindi kwa sababu tulishapoteza mchezo wa kwanza, ushindi unawezekana kesho (leo)," alisema Abdulmutik.

## Yanga SC yaiuzia silaha Azam

INATOKA UK. 24

tika maboresho ya kikosi chao na wanasajili mchezaji ambaye anaonekana ataisadia timu hiyo.

"Kocha Youssouph Dabo anaendelea na kazi ya kuboresha kikosi hivyo mashabiki watarajie chochote katika kikosi hicho, tumedhamiria kufanya vizuri katika msimu ujao, so tusibiri kama huyomchezaji amejiunga na sisi au anatarajia kujiunga watu watajua tu" alisema Zaka.

Wakati huo huo, Zaka alisema kikosi cha timu hiyo kinatarajiwa kurejea nchini leo saa 7:00 mchana kikitokea Tunisia walipokuwa wameenda kuweka kambi kujiandaa na msimu mpya.



## Kibu apagawa na ubora wachezaji wapya Simba

INATOKA UK. 24

"Nataka niwaambie tu wanachana na mashabiki wa Simba waniamini mimi, lile 'pira' biriani limerudi, halafu lingine linaitwa 'pira' Uturuki, pia kuna samba la kocha Robertinho (Roberto Oliveria), hilo ndiyo wataiinjoi zaidi," alisema mchezaji huyo.

Kibu ambaye alifunga mabao mawili katika mechi tatu za kirafiki za kimataifa walizocheza Uturuki aliwataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kufurika kwa wingi siku ya Simba Day ambapo mbali na burudani zingine kuna mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Power Dynamos ya Zambia.

"Nawaamini Wanasimba, najua watakuja siku hiyo kwa wingi na wataujaza uwanja, hawatoondoka kwa huzuni, watainjoi kwa kile tutakachokionyesha," alisema Kibu.

Kikosi cha Simba kinatarajiwa kurejea nchini Agosti Mosi tayari kwa ajili ya maadhimisho ya tamasha la Simba Day pamoja na msimu mpya wa ligi kuu utakaoanza Agosti 15.

Kabla ya kuanza msimu mpya, Simba itacheza mchezo wa kusaka Ngao ya Jamii dhidi ya

# Michezo

Jumapili Julai 30, 2023

Nipashe




**Man Utd yakataa kumuuza Maguire** UK. 21



Aliyekuwa kuingo wa Yanga, Yanick Bangala (kushoto) akisaini mkataba wa kujiunga na klabu ya Azam jana jijini Dar es Salaam, kulia ni Afisa Mwandamizi wa klabu hiyo Abubakar Mapwisa. **PICHA: AZAM FC**

# YANGA YAIUZIA SILAHA AZAM FC

**Na Saada Akida**

●●● Yamruhusu Bangala kujiunga nayo, yajivunia uwepo wa mchezaji atakayeziba nafasi yake huku ikipokea....

UONGOZI wa klabu ya Yanga umekubali kumuachia kiungo wake Yanick Bangala kujiunga na klabu ya Azam FC kwa dau la shilingi milioni 100, imefahamika.

Yanga hawakumtambulisha mchezaji huyo bora wa ligi kuu (MVP) msimu wa 2021/2022 kwanye kilele cha tamasha lao la mwananchi lililofanyika wiki iliyopita pamoja na Shaban Djuma ambapo taarifa za awali zilieleza wawili hao walikuwa na mgogoro na uongozi wa klabu hiyo.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema uongozi wa timu hiyo umekubali kumuachia kiungo huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kujiunga na Azam hasa baada ya kufanikiwa kupata mrithi wake kwenye kikosi hicho ambaye ni Pacome Zouzoua.

**Awali Yanga ilitaka kuwatoa kwa mkopo wachezaji hao kwenda Singida Fountain Gate lakini wakongo hao waligomea maamuzi hayo.**

Mmoja wa viongozi wa Yanga alisema Bangala yupo kwenye hatua za mwisho kutangazwa kuwa mchezaji wa Azam hasa baada ya kuelezwa ukweli kuwa hayupo kwenye mipango ya kocha Miguel Gamondi.

"Bangala yuko kwenye hatua ya mwisho kukamilisha usajili wake na kwenda Azam FC na baada ya kukamilika watamtambulisha kwa sababu tumemueleza kuwa hayuko kwenye mipango ya Kocha Gamondi, hata kwa Djuma pia, lakini kwa Bangala tayari Azam wameafikiana na Yanga kuhusu malipo" alisema kiongozi huyo.

Kiongozi huyo alisema anaamini taarifa rasmi itatolewa klabu kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili usiku wa leo.

Mkataba wa Bangala na Yanga umebakisha mwaka mmoja kumalizika.

Kwa upande wake uongozi wa Azam FC kupitia kwa Ofisa habari wake Thabit Zacharia 'Zaka' alisema bado wapo ka-

INAENDELEA UK. 23

## Kibu apagawa na ubora wachezaji wapya Simba

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa klabu ya Simba, Kibu Denis ameonyesha kufurahishwa mno na viwango vya wachezaji wapya Aubin Kramo, Willy Onana, Che Fondon Malone na Fabrice Ngoma akisema ni vya hali ya juu, huku akiwataka wanachama na mashabiki kufurika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa siku ya kilele cha tamasha la Simba Day ili kuthibitisha kile anachokisema.

Kibu, ambaye wakati mwingine huchezeshwa kama mshambuliaji wa kati amesema kwa muda ambao wamekaa nao kambini nchini Uturuki, vitu wanavyoonyesha wachezaji hao si vya kawaida na ana uhakika wataisaidia Simba kufanya vizuri kwenye Ligi kuu na mshindano ya kimataifa.

"Wanachana na mashabiki wa Simba safari hii wataburudika sana, kuanzia Simba Day watapata vitu adimu, yaani mbali na sisi wachezaji wa zamani ambao wanatufahamu, lakini kuna hao wapya kina Kramo, Malone, Ngoma, Onana wana vitu vya ajabu hao, wana vitu vikali kiasi kwamba ukiwalinganisha na hata baadhi ya wachezaji tunaowaona kwenye ligi mbalimbali barani Ulaya, yaani kama ni wale wale tu hakuna utofauti," alisema Kibu ambaye yupo na kikosi cha timu hiyo kambini nchini Uturuki.

Alisema msimu huu wanachama na mashabiki wa Simba watarajie aina ya soka ambalo walilizoea misimu miwili iliyopita ambalo lilikuwa likiitwa 'biriani', likifananishwa na aina hiyo ya chakula.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >